JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# FUNGU 35

# OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA

**TAARIFA YA UTENDAJI KAZI YA NUSU MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

**(JANUARI - JUNI, 2023)**

S.L.P 1733,

DODOMA

JULAI, 2023

## YALIYOMO


ORODHA YA MAJEDWALI .......... iv

ORODHA YA CHATI .......... v

MAELEZO MAFUPI KUTOKA KWA MKURUGENZI WA MASHTAKA .......... vi

MAELEZO MAFUPI KUTOKA KWA NAIBU MKURUGENZI WA MASHTAKA .......... vii

MUHTASARI .......... 1

*1. UTANGULIZI .......... 3*

*1.1. Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka .......... 3*

*1.2. Muundo wa Ofisi .......... 4*

*1.3. Dira na Dhima .......... 5*

*1.4. Maadili ya Msingi .......... 5*

*2. MALENGO KWA MWAKA 2022/2023 .......... 5*

*3. MWENENDO WA BAJETI NA MATUMIZI KWA NUSU MWAKA KUANZIA JANUARI, 2023 HADI JUNI, 2023 MWAKA WA FEDHA 2022/2023 .......... 6*

*3.1. Makadirio ya Fedha za Matumizi ya Kawaida .......... 6*

*3.1.1. Makadirio ya Fedha za Mishahara (PE) .......... 6*

*3.1.2. Makadirio ya Matumizi Mengineyo (OC) .......... 6*

*3.2. Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo .......... 7*

*3.3. Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli .......... 7*

*4. MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI .......... 7*

*4.1. Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Upelelezi .......... 7*

*4.1.1. Majalada Yaliyoshughulikiwa kutoka Vyombo vya Upelelezi .......... 7*

*4.1.2. Uundwaji wa Vikosi Kazi Maalum Kusimamia Upelelezi .......... 8*

*4.2. Uendeshaji wa Kesi za Jinai .......... 9*

*4.2.1. Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi .......... 9*

*4.2.2. Mahakama za Watoto .......... 12*

*4.2.3. Mahakama Kuu .......... 15*

*4.2.4. Mahakama ya Rufani .......... 21*

4.2.5. Faini Zilizotozwa na Mali Zilizotaifishwa ........ 23
4.3. Ukaguzi wa Magereza na Vituo vya Polisi ........ 24
4.4. Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi ........ 24
4.5. Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika Makosa ya Jinai ........ 26
4.5.1. Ushirikiano wa kitaifa ........ 26
4.5.2. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ........ 31
4.6. Kuunganisha Mifumo ya Kukusanya, Kuchakata na Kutunza Taarifa za Masuala ya Uendeshaji wa Mashtaka katika Taasisi za Haki Jinai ........ 38
4.7. Kuimarisha Huduma za Mashtaka ........ 39
4.7.1. Maendeleo ya Rasilimali Watu ........ 39
4.7.2. Kushughulikia Malalamiko Yaliyowasilishwa katika Ofisi ........ 39
4.7.3. Uratibu na Usimamizi wa Jukwaa la Haki Jinai ........ 41
4.7.4. Vikao Kazi kati ya Menejimenti na Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa ........ 41
4.7.5. Ukaguzi wa Shughuli za Mashtaka ........ 42
4.7.5.1. Ukaguzi wa Ofisi za Mikoa ........ 42
4.8. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ........ 43
4.8.1. Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Mikoa Kumi (10) ........ 43
4.8.2. Utekelezaji wa Programu ya Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania ........ 45
4.8.3. Utekelezaji wa Mradi wa Haki Mtoto ........ 46
5. MAFANIKIO ........ 47
6. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI ........ 47
i. Ufinyu wa Bajeti ........ 48
ii. Usalama kwa Watumishi ........ 48
iii. Upungufu wa Rasilimali Watu ........ 48
iv. Maslahi Duni kwa Watumishi ........ 48
v. Upungufu wa Vitendea Kazi na Majengo ........ 48
vi. Kuongezeka kwa aina Mpya ya Uhalifu na Matukio Yanayohatarisha Usalama wa Wananchi ........ 49

*vii.* *Ulinzi kwa Watoa Taarifa na Mashahidi* ..... *49*

*7.* *MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA* ..... *49*

*8.* *HITIMISHO* ..... *50*

Kiambatisho Na. 1: Muundo uliopitishwa wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ..... 51

Kiambatisho Na. 2: Taarifa ya Magereza na Vituo vya Polisi Vilivyotembelewa Julai, 2022 hadi Disemba, 2022 ..... 52

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Mwenendo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Kipindi cha Januari hadi Juni, 2023 ..... 6
Jedwali 2: Mwenendo wa Fedha za Maendeleo kwa kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 ..... 7
Jedwali 3: Majalada Yalipokelewa na Kushughulikiwa kutoka Vyombo vya Upelelezi ..... 8
Jedwali 4: Kesi zilizoendeshwa – Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ..... 10
Jedwali 5: Jinsi kesi zilivyokamilika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ..... 11
Jedwali 6: Kesi zilizoendeshwa - Mahakama ya Watoto ..... 13
Jedwali 7: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Mahakama ya Watoto ..... 14
Jedwali 8: Kesi zilizoendeshwa - Vikao vya Mahakama Kuu ..... 15
Jedwali 9: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Vikao vya Mahakama Kuu ..... 16
Jedwali 10: Kesi zilizoendeshwa - Vikao vya Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ..... 17
Jedwali 11: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Vikao vya Mahakama Kuu - Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ..... 18
Jedwali 12: Kesi za Rufaa na Maombi zilizoendeshwa - Mahakama Kuu ..... 20
Jedwali 13: Jinsi Kesi za Rufaa na Maombi zilivyokamilika - Mahakama Kuu ..... 20
Jedwali 14: Kesi za Rufaa na Maombi zilizoendeshwa - Mahakama ya Rufani ..... 20
Jedwali 15: Jinsi Kesi za Rufaa na Maombi Zilivyokamilika ..... 21
Jedwali 16: Fedha zilizokusanywa kutokana na Faini katika makosa mablimbali – Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ..... 23
Jedwali 17: Orodha ya Waendesha Mashtaka Ki-Taasisi/Ofisi na Mikoa ..... 24
Jedwali 18: Taarifa ya Barua za Malalamiko ..... 38

**ORODHA YA CHATI**

Chati 1: Jinsi kesi zilivyokamilika katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi kwa Asilimia ..... 12
Chati 2: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Mahakama ya Watoto kwa Asilimia..... 14
Chati 3: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Vikao vya Mahakama Kuu kwa Asilimia..... 16
Chati 4: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Vikao vya Mahakama Kuu - Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa Asimilia ..... 18
Chati 5: Jinsi Kesi za Rufaa na Maombi zilivyokamilika- Mahakama ya Rufani kwa Asilimia ..... 22

## MAELEZO MAFUPI KUTOKA KWA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) iliundwa kufuatia mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanyika Februari, 2018, kwa Hati Idhini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Na. 49 la mwaka 2018. Mabadiliko haya yaliifanya iliyokuwa Divisheni ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Ofisi huru inayojitegemea na yenye Mamlaka kamili. Mabadiliko haya yalilenga kuongeza ufanisi na tija katika kuratibu shughuli za upelelezi zinazofanywa na vyombo vya upelelezi/uchunguzi na uendeshaji wa kesi za jinai.

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka akisaidiwa na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka na inatekeleza majukumu kupitia Divisheni Sita (6), Vitengo Saba (7), Sehemu Kumi na Nane (18) na Ofisi za Mikoa ya Kimashtaka 30 na Wilaya 94.

Dira ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni *Haki, Amani na Usalama kwa Maendeleo ya Taifa*. Aidha, Dira hii, inazingatia Dhima inayotaka *kushirikiana na wadau kuendesha kesi za jinai bila woga, upendeleo au ubaguzi ili kuhakikisha Haki, Amani na Usalama vinatamalaki katika jamii.*

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka Sura ya 430 marejeo ya mwaka 2022, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inatakiwa kutoa taarifa zake za utekelezaji wa majukumu kwa Waziri wa Katiba na Sheria kila baada ya nusu mwaka. Kutokana na hitaji hilo la kisheria, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inatoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023. Kwa ujumla, Ofisi imetekeleza majukumu kwa ufanisi na kuridhisha kwa kipindi husika.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Watumishi wa OTM, Wadau wa Haki Jinai na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Sylvester Anthony Mwakitalu

**MKURUGENZI WA MASHTAKA**

## MAELEZO MAFUPI KUTOKA KWA NAIBU MKURUGENZI WA MASHTAKA

Katika kipindi cha Mwezi Januari, 2023 hadi Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendelea kutekeleza majukumu kama yalivyoainishwa katika Mpango Kazi wa mwaka wa Fedha 2022/2023. Ofisi imeweza kutekeleza majukumu yake ikiwemo kushughulikia majalada kutoka vyombo vya upelelezi, uendeshaji wa kesi za jinai katika Mahakama zote, uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi, ukaguzi wa Magereza na Vituo vya Polisi, utekelezaji wa program ya utenganishaji wa shughuli za mashtaka na upelelezi na kuendeleza ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika haki jinai.

Ofisi imeweza kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi na kupata mafanikio ikiwemo kupunguza mlundikano wa kesi katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani na kupunguza msongamano wa mahabusi katika magereza nchini. Mafanikio mengine ni kusogeza huduma kwa jamii kwa kuongeza Ofisi za Mashtaka katika baadhi ya Wilaya nchini, kuokoa mali za Serikali na kupungua kwa malalamiko kwa Serikali. Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika uendeshaji na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Miongoni mwa changamoto hizo ni ufinyu wa bajeti, ukosefu wa majengo ya Ofisi, upungufu wa rasilimali watu, kuibuka kwa aina mpya ya uhalifu, ulinzi kwa watoa taarifa na usalama mdogo na maslahi duni kwa watumishi. Mbali na changamoto hizo, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu ya msingi kulingana na rasilimali zilizopo.

Ni matumaini kuwa Serikali itaendelea na jitihada za kuimarisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili iweze kutekeleza azma ya kuongeza ufanisi na tija katika usimamizi wa haki jinai kwa lengo la kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini.

Ushirikiano uliopo kati ya watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wadau wa haki jinai ndiyo nguzo iliyotuwezesha kutekeleza majukumu kwa ufasaha. Halikadhalika, nidhamu na kujituma kwa watumishi kufanya kazi kwa bidii kumeongeza tija na mabadiliko makubwa katika utendaji. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wadau wote wa haki jinai nchini kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa.

Joseph Sebastian Pande

**NAIBU MKURUGENZI WA MASHTAKA**

## MUHTASARI

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) iliendelea kutekeleza majukumu ya msingi kwa kuzingatia Mpango Kazi kwa kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023. Mpango Kazi wa Ofisi umeainisha malengo Nane (8) ya utekelezaji ambayo yanajumuisha Kuboresha huduma kwa watumishi kwa ajili ya kupunguza maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa UKIMWI; Kutekeleza Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kupambana na Rushwa; kuimarisha Mfumo wa Utaifishaji, Usimamizi na Urejeshwaji wa Mali zinazohusiana na Uhalifu; kuimarisha Uratibu na Usimamizi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai; kuimarisha Uendeshaji Mashtaka na Usimaizi wa Kesi za Jinai; Kuimarisha Ushirikiano katika Masuala ya Kisheria Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; Kuboresha Mazingira ya Kazi na Vitendea Kazi; na Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi na Utendaji Kazi.

Katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi ilipokea kutoka Wizara ya Fedha na Mipango jumla ya **Shilingi 17,929,924,066.70** kwa ajili ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 7,274,375,500** ilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi sawa **asilimia 100** ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi husika na kiasi cha **Shilingi 10,655,548,566.70** kilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na **asilimia 100** ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa. Kwa upande wa matumizi ya Maendeleo Ofisi ilipokea jumla ya **Shilingi 3,624,805,962.73** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 95.5** ya bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa kipindi husika.

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, jumla ya majalada 2,471 yalivuka na majalada 10,382 yalipokelewa kutoka vyombo vya upelelezi na kufanya jumla ya majalada kuwa 12,853. Kati ya hayo, Majalada 8,786 sawa na asilimia 68.4 yaliandaliwa hati za mashtaka na kupewa ridhaa ya mashtaka; majalada 812 sawa na asilimia 6.3 yalifungwa na majalada 2,040 sawa na asilimia 15.9 ambayo ni wastani wa majalada 68 kwa kila mkoa yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi. Aidha, majalada 1,215 sawa na asilimia 9.5 bado yanaendelea kufanyiwa kazi.

Katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi, jumla ya kesi 12,801 zilivuka kutoka mwezi Disemba, 2022. Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni,

2023, kesi 10,169 zilifunguliwa na kufanya jumla ya kesi kuwa 22,970. Kati ya kesi hizo, kesi 10,773 sawa na asilimia 46.9 zilisikilizwa na kutolewa uamuzi na kesi 12,197 sawa na asilimia 53.1 ya kesi zote zilizokuwepo zilikuwa zinaendelea mahakamani. Kati ya kesi zilizokwisha mahakamani, kesi 6,623 sawa na asilimia 61.5 washtakiwa walitiwa hatiani na kupewa adhabu za aina mbalimbali ikiwemo vifungo gerezani, kutumikia huduma kwa jamii, faini na kutaifisha mali.

Katika Mahakama za Watoto (*Juvenile Courts*), jumla ya kesi 714 ziliendeshwa ambapo, kesi 258 zilikuwepo hadi Disemba, 2022 na kesi 456 zilifunguliwa kati ya Januari hadi Juni, 2023. Kati ya kesi 714, kesi 355 sawa na asilimia 49.7 ya kesi zilizokuwepo zilihitimishwa mahakamani na kesi 359 sawa na asilimia 50.3 zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji katika Mahakama za Watoto nchini.

Katika ngazi ya Mahakama Kuu jumla ya kesi 2,720 zilisikilizwa, ambapo kesi 2,151 zilikuwa zimevuka Disemba, 2022 na kesi 569 zilifunguliwa kati ya Januari hadi Juni, 2023. Kati ya hizo, kesi 607 zilikwisha na kesi 2,113 zilikuwa zinaendelea Mahakamani. Aidha, jumla ya rufaa na maombi 2,148 yaliendeshwa Mahakama Kuu na kati ya hizo, rufaa na maombi 803 yalisikilizwa na kutolewa maamuzi na 1,345 zinaendelea mahakamani.

Jumla ya Kesi 58 ziliendeshwa katika Mahakama Kuu – Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na kesi 19 zilimalizika na kesi 39 zinaendelea mahakamani na zipo kwenye hatua mbalimbali za usikilizwaji.

Katika kipindi husika (Januari – Juni, 2023) kiasi cha **Shilingi 725,690,880** kililipwa mahakamani kama faini katika **kesi 2,836** na kiasi cha **Shilingi 636,413,783.61** zililipwa kama faini na fidia na watuhumiwa waliokili makosa kwa njia ya makubaliano (*Plea-Bargaining*). Aidha, mali mbalimbali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu ama zilizotumika kutenda uhalifu zilitaifishwa kuwa mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mali hizo ni pamoja na magari 11, pikipiki 64, viwanja saba (7), mifugo (ng’ombe 2,403, mbuzi 19 na kondoo 77) na fedha taslimu **Shilingi 1,455,698,000** na **Dola za Kimarekani 2,064**.

## 1. UTANGULIZI

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) iliundwa kufuatia mabadiliko ya kimuundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanyika mwaka 2018, kwa Hati idhini ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Na. 49 la mwaka 2018. Hati Idhini hiyo, iliifanya iliyokuwa Divisheni ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Ofisi huru inayojitegemea na yenye Mamlaka kamili. Mabadiliko yalilenga kuongeza ufanisi na tija katika uendeshaji wa kesi za jinai na kuratibu shughuli za upelelezi zinazofanywa na vyombo vya upelelezi. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inatekeleza majukumu kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) 2020/2021 hadi 2024/2025.

### 1.1. Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Pamoja na mambo mengine majukumu ya msingi ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) ni kama ifuatavyo;

i. Kufanya uamuzi wa kufungua au kutofungua mashtaka;

ii. Kusimamia uendeshaji wa mashtaka yote ya jinai nchini isipokuwa yale yaliyo katika Mahakama za kijeshi;

iii. Kusitisha kesi iliyofunguliwa mahakamani na mtu au mamlaka yoyote kwa kuzingatia matakwa ya sheria;

iv. Kuchukua na kuendesha mashtaka yaliyofunguliwa mahakamani na mtu au mamlaka yoyote kwa kuzingatia matakwa ya sheria;

v. Kukata rufaa au kufungua maombi au kujibu rufaa au maombi kwa niaba ya Jamhuri;

vi. Kusimamia na kuratibu shughuli za upelelezi pamoja na kuratibu shughuli zinazofanywa na vyombo vya upelelezi/chunguzi;

vii. Kuagiza chombo chochote kinachohusika na upelelezi wa makosa ya jinai kuendesha upelelezi kuhusiana na taarifa zenye mwelekeo wa jinai zilizofika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

viii. Kukagua magereza na mahali popote wanapohifadhiwa wahalifu kwa mujibu wa sheria;

ix. Kusimamia kazi za Jukwaa la Haki Jinai la Taifa, Mikoa na Wilaya;

x. Kutoa ushauri wa kisheria kwa mamlaka mbalimbali katika masuala ya Jinai;

xi. Kuendesha na kusimamia kesi zinazohusiana na utaifishwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu;

xii. Kutoa miongozo mbalimbali kwa wadau wa Haki Jinai kuhusu upelelezi na uendeshaji wa mashtaka;

xiii. Kuratibu mashauri yanayohusiana na uhamishwaji wa wahalifu kutoka ndani na nje ya nchi na kusaidia mamlaka za ndani na nje katika masuala ya Jinai;

xiv. Kuelekeza na kushiriki kwenye utafiti wa kifo *(inquests)*; na

xv. Kuunda kikosi kazi kwa ajili ya kuchunguza na kupeleleza suala mahsusi la kijinai kadri atavyoona inafaa.

### 1.2. Muundo wa Ofisi

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ina Divisheni Sita (**6**)**,** Vitengo Saba (**7**), Sehemu **18** na Ofisi za Mikoa **30** na Wilaya 64. Ona ***Kiambatisho Na. 1*** kinaonesha Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Divisheni na Vitengo ni kama ifuatavyo;

i. Divisheni ya Makosa ya Udanganyifu, Utakatishaji Fedha na Rushwa;
ii. Divisheni ya Utaifishaji wa Mali, Makosa yanayovuka Mipaka na Uhalifu wa Kupangwa**;**
iii. Divisheni ya Kusimamia Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi**;**
iv. Divisheni ya Usimamizi na Uratibu wa Kesi za Jinai**;**
v. Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu;
vi. Divisheni ya Mipango;
vii. Kitengo cha Fedha na Uhasibu;
viii. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;
ix. Kitengo cha Ununuzi na Ugavi;
x. Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;
xi. Kitengo cha Mawasiliano Serikalini;
xii. Kitengo cha Utafiti na Maktaba; na
xiii. Kitengo cha Masjala ya Sheria.

### 1.3. Dira na Dhima

Ili kuweza kutekeleza majukumu kwa ufanisi na weledi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) imejiwekea Dira na Dhima. Dira ya OTM ni ***"Haki, Amani na Usalama kwa Maendeleo ya Taifa"*** na Dhima ni ***"Kushirikiana na wadau kuendesha kesi za jinai bila woga, upendeleo au ubaguzi ili kuhakikisha Haki, Amani, na Usalama vinatamalaki katika jamii".***

### 1.4. Maadili ya Msingi

Ili kuweza kufikia malengo yaliyobainishwa na Dira na Dhima ya Ofisi, maadili haya ya msingi yanazingatiwa, ambayo ni;

i. Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuwajibika kwa Serikali na Umma kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yao kwa wakati;
ii. Watumishi wa Ofisi kujenga imani na uaminifu kwenye jamii ambayo wanaihudumia;
iii. Watumishi wa Ofisi kuzingatia maadili na kutowavumilia watakaojihusisha na vitendo vya rushwa na ubadhirifu;
iv. Watumishi kuzingatia weledi, utaalamu na kujituma katika utoaji huduma wakati wote wanapokuwa ofisini na nje ya ofisi; na
v. Kufanyakazi kwa umoja na kwa kuheshimiana ili kutoa huduma bora kwa watu wote***.***

## 2. MALENGO KWA MWAKA 2022/2023

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imepanga kutekeleza malengo ya kimkakati yafuatayo;

i. Kuboresha Huduma kwa watumishi kwa ajili ya kupunguza maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa UKIMWI;

ii. Kutekeleza Mkakati na Mpango kazi wa Taifa wa Kupambana na Rushwa;

iii. Kuimarisha uendeshaji mashtaka na usimamizi wa kesi za jinai;

iv. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa upelelezi wa makosa ya jinai;

v. Kuimarisha mfumo wa utaifishaji, usimamizi na urejeshwaji wa mali zinazotokana na uhalifu;

vi. Kuimarisha ushirikiano wa masuala ya kisheria baina ya taasisi, kitaifa na kimataifa;

vii. Kuimarisha mfumo wa usimamizi na utendaji kazi; na

viii. Kuboresha vitendea kazi na mazingira ya kazi ili kuleta tija na ufanisi.

## 3. MWENENDO WA BAJETI NA MATUMIZI KWA NUSU MWAKA KUANZIA JANUARI, 2023 HADI JUNI, 2023 MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 3.1. Makadirio ya Fedha za Matumizi ya Kawaida

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 jumla ya **Shilingi 17,929,924,066.70** zilipangwa kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, jumla ya **Shilingi 17,929,924,066.70** zilipokelewa na kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 100** ya makadirio kwa kipindi husika.

#### 3.1.1. Makadirio ya Fedha za Mishahara (PE)

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, jumla ya **Shilingi 7,274,375,500.00** zilipangwa kutumika kwa ajili ya kulipa Mishahara ya Watumishi (PE). Hadi kufikia 30 Juni, 2023 jumla ya kiasi cha **Shilingi 7,274,375,500.00** kilipokelewa na kutumika kulipa mishahara sawa na **asilimia 100** ya makadirio kwa kipindi husika.

#### 3.1.2. Makadirio ya Matumizi Mengineyo (OC)

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 kiasi cha **Shilingi 10,655,548,566.70** kilipangwa kutumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla ya **Shilingi 10,655,548,566.70** sawa na **asilimia 100** zilipokelewa na kutumika kwenye Matumizi Mengineyo. Kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1.

**Jedwali 1: Mwenendo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Kipindi cha Januari - Juni, 2023**

| Maelezo | Bajeti iliyoidhinishwa (2022/2023) | Kiasi Kilichopokelewa (Januari - Juni, 2023) | Kiasi Kilichotumika (Januari - Juni, 2023) |
|---|---|---|---|
| Mishahara (PE) | 14,548,751,000.00 | 7,274,375,500.00 | 7,274,375,500.00 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 22,068,944,000.00 | 10,655,548,566.70 | 10,655,548,566.70 |
| **Jumla** | **36,617,695,000.00** | **17,929,924,066.70** | **17,929,924,066.70** |

### 3.2. Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Maendeleo

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 jumla ya **Shilingi 3,624,805,962.73** kutoka Ndani na Nje ya nchi zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kiasi cha **Shilingi 3,461,678,364.90** kilitolewa na kutumika sawa na asilimia 95.5 ya makadirio ya kipindi husika. (Jedwali Na. 2).

**Jedwali 2: Mwenendo wa Fedha za Maendeleo kwa kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023**

| Maelezo | Bajeti Iliyoidhinishwa 2022/2023 | Kiasi Kilichopokelewa (Januari – Juni, 2023) | Kiasi Kilichotumika (Januari - Juni, 2023) |
|---|---|---|---|
| Fedha za Ndani | 8,000,000,000.00 | 3,157,933,560.56 | 3,157,933,560.56 |
| Fedha za Nje | 630,000,000.00 | 466,872,402.17 | 466,872,402.17 |
| **Jumla** | **8,630,000,000.00** | **3,624,805,962.73** | **3,624,805,962.73** |

### 3.3. Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 OTM ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 56,400,000.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Miongoni mwa vyanzo hivyo ni pamoja na malipo ya kodi ya pango na marejesho ya mishahara kwa watumishi wanaokatisha ajira zao kwa muda wa masaa 24. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Ofisi ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 56,400,000.00** sawa na **asilimia 100**.

## 4. MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI

Katika kipindi cha Nusu Mwaka kinachoanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023 hali halisi ya utekelezaji wa majukumu katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023 ilikuwa kama ifuatavyo:

### 4.1. Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Upelelezi

#### 4.1.1. Majalada Yaliyoshughulikiwa kutoka Vyombo vya Upelelezi

Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023 OTM ilitekeleza jukumu la uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi zinazofanywa na vyombo vya upelelezi/chunguzi. Katika kipindi husika jumla ya majalada 12,853 kutoka vyombo vya upelelezi yalishughulikiwa. Kati ya majalada hayo, majalada 2,471

yalikuwepo toka Disemba 31 na majalada 10,382 yalifunguliwa katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2023 na kufanya jumla ya majalada 12,853.

Kati ya majalada 12,853, majalada 8,786 sawa na asilimia 68.4 yaliandaliwa hati za mashtaka na majalada 812 sawa na asilimia 6.3 yalifungwa. Aidha, majalada 2,040 sawa na asilimia 15.9 yalirejeshwa kwa upelelezi zaidi. Katika kipindi husika jumla ya majalada 11,638 sawa na asilimia 90.5 ya majalada yote yaliyokuwepo yalifanyiwa kazi. Vilevile, majalada 1,215 sawa na asilimia 9.5 ya majalada yote yaliyopokelewa yalikuwa yanaendelea kufanyiwa kazi. (Jedwali 3).

**Jedwali 3: Majalada Yalipokelewa na Kushughulikiwa kutoka Vyombo vya Upelelezi**

| Na. | Taasisi Chunguzi | Yaliyokuwepo hadi 31 Dec, 2022 | Yaliyopokelewa | Jumla | Yaliyoandaliwa Mashtaka | Yaliyofungwa | Yaliyorudishwa kwa Upelelezi | Yanayoendelea kufanyiwa kazi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TAKUKURU | 148 | 563 | **711** | 287 | 71 | 168 | **185** |
| 2 | Polisi-Makao Makuu | 35 | 19 | **54** | 30 | 3 | 14 | **7** |
| 3 | Polisi-Mkoani RCOs | 978 | 1,649 | **2,627** | 1,628 | 222 | 568 | **209** |
| 4 | Polisi- Wilayani (OC CIDs) | 700 | 5,575 | **6,275** | 4,096 | 431 | 1,086 | **662** |
| 5 | Polisi- Trafiki (DTO) | 452 | 2,307 | **2,759** | 2,410 | 78 | 183 | **88** |
| 6 | Mamlaka-Dawa za Kulevya | 16 | 119 | **135** | 79 | 5 | 8 | **43** |
| 7 | Idara ya Uhamiaji | 7 | 100 | **107** | 89 | 2 | 11 | **5** |
| 8 | Taasisi Nyingine | 135 | 50 | **185** | 167 | 0 | 2 | **16** |
| **Jumla** | | **2,471** | **10,382** | **12,853** | **8,786** | **812** | **2,040** | **1,215** |

### 4.1.2. Uundwaji wa Vikosi Kazi Maalum Kusimamia Upelelezi

Uratibu na usimamizi wa upelelezi ulifanyika katika kipindi husika katika matukio makubwa yaliyohitaji maelekezo kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Lengo ni kushirikiana kwa ukaribu na vyombo vya upelelezi/uchunguzi ili kuboresha ushahidi na hivyo kuleta matokeo chanya pindi kesi zinapowasilishwa Mahakamani. Katika kutekeleza jukumu hili Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifanya kazi zifuatazo;

i. Januari, 2023 hadi 31 March, 2023 Kikosi Kazi Ulinzi kwa Watoto dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu (AHTCP/TF) kilishughulikia mashauri mbalimbali ya ubakaji na ulawiti. Kikosi Kazi kilipokea jumla ya kesi 146 kati ya hizo 87 ni kesi za kubaka, 41 ni kesi za kulawiti, saba (7) ni kesi za kuwapa mimba wanafunzi, moja (1) ni kesi ya

usafirishaji haramu wa binadamu na kesi mbili (2) za kudhini na maharimu. Jumla ya manusura/wahanga 164 walipatikana ambapo wote walipatiwa msaada wa kisaikolojia na ulinzi. Wahanga 34 walipelekwa kwenye nyumba salama na wengine kuunganishwa na familia zao. Jumla ya kesi 69 zimefunguliwa mahakamani ambapo kesi 56 zinaendelea mahakamani katika hatua mbalimbali na kesi 13 tayari zimeamuliwa; na

ii. Kuanzia tarehe 22 Mei, 2023 hadi 22 Juni, 2023 Kikosi Kazi cha Ulinzi kwa Watoto dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu (AHTCP/TF) kilifanya ziara katika mikoa tisa (9). Lengo la ziara ilikuwa kupitia kesi zinazohusu ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto na usafirishaji haramu dhidi ya binadamu na pia kuainisha changamoto na mapungufu yanayojitokeza katika kusimamia kesi hizo katika hatua ya upelelezi, uendeshaji mashtaka na namna ya kuwahudumia manusura walioathirika. Kazi hii ilisaidia Kikosi Kazi kuendesha mashauri hayo pamoja nakupata takwimu sahihi za kesi zilizotajwa hapo juu;

## 4.2. Uendeshaji wa Kesi za Jinai

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliratibu na kuendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kama inavyojieleza hapa chini.

### 4.2.1. Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 Ofisi iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya na Hakimu mkazi kama ifuatavyo;

#### i. Kesi Zilizoendeshwa

Jumla ya kesi za jinai 22,970 ziliendeshwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi nchini. Kati ya kesi hizo, kesi 12,801 zilikuwepo hadi 31 Disemba, 2022 sawa na asilimia 55.7 na kesi 10,169 zilifunguliwa kati ya Januari na Juni, 2023 sawa na asilimia 44.3 ya kesi zote katika kipindi kinachofanyiwa tathmini.

Katika kipindi husika, kesi 10,773 sawa na asilimia 46.9 zilihitimishwa mahakamani na kesi 12,197 sawa na asilimia 53.1 ya kesi zilizoendeshwa, zilikuwa zinaendelea mahakamani zikiwa katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. (Jedwali Na. 4).

**Jedwali 4: Kesi zilizoendeshwa – Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi**

| Na. | Aina ya Makosa | Zilizokuwepo hadi 31 Disemba, 2022 | Zilizofunguliwa | Jumla | Zilizokwisha Mahakamani | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Nyara za Serikali | 1,082 | 302 | **1,384** | 391 | 993 |
| 2 | Kesi za Maliasili nyinginezo | 487 | 491 | **978** | 600 | 378 |
| 3 | Dawa za Kulevya | 1,712 | 619 | **2,331** | 903 | 1,428 |
| 4 | Madini | 59 | 30 | **89** | 41 | 48 |
| 5 | Udanganyifu | 1,325 | 871 | **2,196** | 727 | 1,469 |
| 6 | Utakasishaji Fedha | 20 | 6 | **26** | 10 | 16 |
| 7 | Uhalifu wa Mtandao | 38 | 23 | **61** | 15 | 46 |
| 8 | Usafirishaji Haramu wa Binadamu | 0 | 5 | **5** | 3 | 2 |
| 9 | Magendo ya Binadamu | 11 | 4 | **15** | 2 | 13 |
| 10 | Unyanganyi wa Kutumia Silaha | 1,005 | 279 | **1,284** | 401 | 883 |
| 11 | Uharamia | 8 | 0 | **8** | 8 | 0 |
| 12 | Kubaka | 2,440 | 804 | **3,244** | 1,260 | 1,984 |
| 13 | Rushwa | 0 | 48 | **48** | 21 | 27 |
| 14 | Mauaji | 607 | 603 | **1,210** | 498 | 712 |
| 15 | Ugaidi | 2 | 0 | **2** | 1 | 1 |
| 16 | Usalama Barabani | 1,404 | 2,036 | **3,440** | 2,453 | 987 |
| 17 | Kuingia na kuishi nchini bila kibali | 198 | 313 | **511** | 450 | 61 |
| 18 | Makosa Mengine | 2,403 | 3,735 | **6,138** | 2,989 | 3,149 |
| **Jumla** | | **12,801** | **10,169** | **22,970** | **10,773** | **12,197** |

### ii. Jinsi Kesi Zilivyohitimishwa

Jumla ya kesi 10,773 zilikamilika mahakamani ambapo, kesi 6,623 sawa na asilimia 61.5 ya kesi zote zilimalizika kwa watuhumiwa kutiwa hatiani. Kesi 502 sawa na asilimia 4.7 zilimalizika kwa kuondolewa Mahakamani na waendesha mashtaka chini ya Kifungu 98 (a) CPA.

Aidha, kesi 1,383 ambayo ni sawa na asilimia 12.8 zilimalizika kwa kufutwa na Mahakama chini ya Kifungu 225(5) CPA na kesi 812 sawa na asilimia 7.5 ya kesi zilikamilika kwa kufutwa na Mawakili wa Serikali chini ya Kifungu cha 91 (1) CPA *(Nolle Prosequi)*.


Halikadhalika, kesi 969 sawa na asilimia 9 zilimalizika kwa watuhumiwa kuachiwa huru chini ya Kifungu 312 (3) CPA (Acquitted), na kesi 407 ambayo ni sawa na asilimia 3.8 zilikamilika kwa kupelekwa Mahakama Kuu chini ya Kifungu 246 CPA kwa ajili ya kusikilizwa.

Vilevile, kesi 56 sawa na asilimia 0.5 zilifutwa chini ya Vifungu 222 na 226 CPA, kesi 12 sawa na asilimia 0.11 zilihitimishwa mahakamani kwa watuhumiwa kufariki dunia na kesi 9 sawa na asilimia 0.1 zilikwisha kwa makubaliano ya watuhumiwa kukiri makosa yao chini ya Kifungu 194A CPA. (Jedwali Na. 5 na Chati Na. 1).

**Jedwali 5: Jinsi kesi zilivyokamilika katika mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi**

| Aina ya Makosa | Kesi zilizoisha kwa Washtakiwa kutiwa hatianichini ya k/f 312 (2) CPA | Kesi zilizoondolewa na Waendesha Mashtaka chini ya k/f 98 (a) CPA | Kesi zilizofutwa na Mahakama chini ya k/f225 (5) CPA | Kesi zilizoondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya k/f 91(1) CPA | Kesi zilizoisha kwa Washtakiwa kuachiwa huruchini ya k/f 312 (3) CPA | Kesi zilizokamilishwa kwenda Mahakama Kuu chini ya k/f 246 CPA | Kesi zilizofutwa chini ya k/f 222 & 226 CPA | Kesi ambazo washitakiwa wamefariki k/f 224A CPA | Kesi zilizoisha kwa makubaliano ya washtakiwa kikiri makossa chini ya k/f 194A CPA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nyara za Serikali | 206 | 7 | 61 | 46 | 64 | 3 | 0 | 0 | 4 |
| Maliasili nyinginezo | 534 | 9 | 22 | 10 | 16 | 7 | 1 | 1 | 0 |
| Dawa za Kulevya | 506 | 38 | 167 | 45 | 122 | 18 | 4 | 2 | 1 |
| Madini | 25 | 0 | 7 | 5 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Udanganyifu | 285 | 76 | 169 | 84 | 102 | 1 | 8 | 1 | 1 |
| Utakasishaji Fedha | 1 | 1 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Uhalifu wa Mtandao | 6 | 0 | 1 | 4 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Usafirishaji wa Binadamu | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magendo ya Binadamu | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Unyanganyi wa Kutumia Silaha | 85 | 22 | 107 | 100 | 86 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Uharamia | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka | 602 | 109 | 246 | 86 | 209 | 0 | 6 | 2 | 0 |
| Rushwa | 19 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Mauaji | 18 | 3 | 3 | 91 | 4 | 351 | 28 | 0 | 0 |
| Ugaidi | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Usalama Barabani | 2,352 | 5 | 34 | 37 | 23 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kuingia na kuishi nchini bila kibali | 439 | 3 | 4 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Makosa Mengine | 1,534 | 229 | 561 | 297 | 333 | 24 | 7 | 4 | 0 |
| **Jumla** | **6,623** | **502** | **1,383** | **812** | **969** | **407** | **56** | **12** | **9** |

**Chati 1: Jinsi Kesi Zilivyokamilika katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi kwa asilimia**




### 4.2.2. Mahakama za Watoto

#### i. Kesi Zilizoendeshwa

Katika Mahakama za Watoto (Juvenile Courts), jumla ya kesi 714 ziliendeshwa ambapo, kesi 258 zilikuwepo hadi Disemba, 2022 na kesi 456 zilifunguliwa kati ya Januari hadi Juni, 2023.

Kati ya kesi 714, kesi 355 sawa na asilimia 49.7 ya kesi zilizokuwepo zilihitimishwa mahakamani na kesi 359 sawa na asilimia 50.3 zipo katika

hatua mbalimbali za usikilizwaji katika Mahakama za Watoto nchini. (Jedwali Na. 6).

**Jedwali 6: Kesi zilizoendeshwa - Mahakama ya Watoto**

| Na. | Aina ya Makosa | Zilizokuwepo hadi 31 Disemba, 2022 | Zilizofunguliwa | Jumla | Zilizokwisha Mahakamani | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dawa za Kulevya | 4 | 13 | **17** | 7 | 10 |
| 2 | Udanganyifu | 7 | 64 | **71** | 46 | 25 |
| 3 | Unyanganyi wa Kutumia Silaha | 8 | 9 | **17** | 2 | 15 |
| 4 | Kubaka | 103 | 162 | **265** | 132 | 133 |
| 5 | Mauaji | 3 | 6 | **9** | 5 | 4 |
| 6 | Ugaidi | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 |
| 7 | Makosa Mengine | 133 | 202 | **335** | 163 | 172 |
| **Jumla** | | **258** | **456** | **714** | **355** | **359** |

### ii. Kesi Zilivyohitimishwa


Katika kipindi husika, jumla ya kesi 355 zilimalizika Mahakamani na kati ya hizo, kesi 272 ambayo ni sawa na asilimia 76.6 zilimalizika kwa watuhumiwa kutiwa hatiani na kesi 16 sawa na asilimia 4.5 zilimazika kwa kuondolewa mahakamani na Waendesha Mashtaka chini ya Kifungu 98 (a) CPA.

Aidha, kesi 20 sawa na asilimia 5.6 zilifutwa mahakamani chini ya Kifungu 225 (5) CPA, na kesi 11 sawa na asilimia 3.1 ziliondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya Kifungu cha 91 (1) CPA, kesi 30 sawa na asilimia 8.5 ziliondolewa mahakamani kwa washtakiwa kuachiwa huru chini ya Kifungu 312 (3) CPA. Aidha, kesi 6 sawa na asilimia 1.7 ya kesi zote zilimalizika kwa kwenda Mahakama Kuu chini ya kifungu 246 CPA kwa usikilizwaji. (Jedwali Na. 7 na Chati Na. 2).

**Jedwali 7: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Mahakama ya Watoto**

| Aina ya Makosa | Kesi zilizoisha kwa Washtakiwa kutiwa hatianichini ya k/f 312 (2) CPA | Kesi zilizoondolewa na Waendesha Mashtaka chini ya k/f 98 (a) CPA | Kesi zilizofutwa na Mahakama chini ya k/f225 (5) CPA | Kesi zilizoondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya k/f 91(1) CPA | Kesi zilizoisha kwa Washtakiwa kuachiwa huru chini ya k/f 312 (3) CPA | Kesi zilizokamilishwa kwenda Mahakama Kuu chini ya k/f 246 CPA | Kesi zilizofutwa chini ya k/f 222 & 226 CPA | Kesi ambazo washitakiwa wamefariki k/f 224A CPA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dawa za Kulevya | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Udanganyifu | 37 | 2 | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Unyanganyi wa Kutumia Silaha | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kubaka | 106 | 6 | 8 | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 |
| Ugaidi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Makosa Mengine | 121 | 7 | 9 | 4 | 21 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **272** | **16** | **20** | **11** | **30** | **6** | **0** | **0** |

**Chati 2: Jinsi Kesi Zilivyokamilika - Mahakama ya Watoto kwa asilimia**




### 4.2.3. Mahakama Kuu

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha kesi za jinai katika Vikao vya Mahakama Kuu, Mahakama Kuu-Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na Rufaa na Maombi Mahakama Kuu kama ifuatavyo;

### A. Vikao vya Mahakama Kuu

#### i. Kesi Zilizoendeshwa

Jumla ya kesi 2,720 zilisikilizwa katika Vikoa vya Mahakama Kuu ambapo kesi 2,151zilikuwa zimevuka Disemba, 2022 na kesi 569 zilifunguliwz kati ya Januari hadi Juni, 2023. Kati ya hizo, kesi 607 zilikwisha na kesi 2,113 zilikuwa zinaendelea Mahakamani. (Jedwali Na. 8).

**Jedwali 8: Kesi zilizoendeshwa - Vikao vya Mahakama Kuu**

| Na. | Aina ya Makosa | Zilizovuka hadi 30 Disemba, 2022 | zilizofunguliwa | Jumla | Zilizokamilika | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dawa za Kulevya | 58 | 12 | **70** | 5 | 65 |
| 2 | Nyara za Serikali | 40 | 1 | **41** | 0 | 41 |
| 3 | Mauaji ya Kukusudia | 1,405 | 389 | **1794** | 410 | 1384 |
| 4 | Mauaji Yasiyo ya Kukusudia | 525 | 142 | **667** | 149 | 518 |
| 5 | Makosa Mengine | 123 | 25 | **148** | 43 | 105 |
| **Jumla** | | **2,151** | **569** | **2,720** | **607** | **2,113** |

### ii. Kesi Zilivyohitimishwa


Katika kipindi husika, jumla ya kesi 607 zilikwisha katika vikao vya Mahakama Kuu na kati ya hizo kesi 420 sawa na asilimia 69.2 washtakiwa walitiwa hatiani, kesi 92 sawa na asilimia 15.2 kesi zilizoondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya Kifungu 91(1) CPA na kesi 40 sawa na asilimia 6.6 washtakiwa waliachiwa huru. Aidha, kesi 49 sawa na asilimia 8.1 watuhumiwa waliamriwa kupelekwa katika Taasisi ya Afya ya Akili (Criminal Lunatic) na kesi 6 sawa na asilimia 1 ziliisha kutokana na washtakiwa kufariki dunia. Hata hivyo, hakukuwa na kesi iliyomalizika kwa watuhumiwa kukiri makosa. (Jedwali Na. 9 na Chati Na. 3).

**Jedwali 9: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Vikao vya Mahakama Kuu**

| Aina ya Makosa | Kesi zilizoisha kwa Watuhumiwa kutiwa hatiani | Kesi zilizoisha kwa Watuhumiwa kuachiwa huru | Kesi zilizoondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya k/f 91(1) CPA | watuhumiwa kuamriwa kupelekwa kwenye taasisi ya afya ya akili (*Criminal Lunatic*) | Kesi zilizofutwa kutokana na watuhumiwa kufariki | Kesi Zilizokamilika kwa Watuhumiwa Kukiri Makosa (Plea Bargaining) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dawa za Kulevya | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Nyara za Serikali | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mauaji ya kukusudia | 249 | 29 | 80 | 46 | 6 | 0 |
| Mauaji Yasiyo ya Kukusudia | 134 | 6 | 7 | 2 | 0 | 0 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Makosa Mengine | 32 | 5 | 5 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **420** | **40** | **92** | **49** | **6** | **0** |

**Chati 3: Jinsi Kesi zilivyokamilika - Vikao vya Mahakama Kuu kwa Asilimia**




## B. Vikao vya Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi

### i. Kesi Zilizoendeshwa

Jumla ya Kesi 68 ziliendeshwa katika ngazi ya Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ambapo kesi 36 zilikuwepo hadi Disemba, 2022 na kesi 32 zilifunguliwa kati ya Januari hadi Juni, 2023. Kati ya kesi hizo, kesi 19 sawa na asilimia 27.9 zilimalizika na kesi 49 sawa na asilimia 72.1 zilikuwa zinaendelea Mahakamani. (Jedwali Na. 10).

**Jedwali 10: Kesi zilizoendeshwa - Vikao vya Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi**

| Na. | Aina ya Makosa | Zilizovuka 31 Disemba, 2022 | Zilizofunguliwa | Jumla | Zilizokamilika | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dawa za Kulevya | 25 | 27 | 52 | 18 | 34 |
| 2 | Nyara za Serikali | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 3 | Rushwa | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| 4 | Makosa ya Udanganyifu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Utakasishaji Fedha | 4 | 4 | 9 | 0 | 8 |
| 6 | Ugaidi | 6 | 1 | 7 | 1 | 6 |
| 7 | Makosa Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | **36** | **32** | **68** | **19** | **49** |

### ii. Kesi Zilivyohitimishwa


Katika kipindi husika, jumla ya kesi 19 zilimalizika na kati ya hizo, kesi 10 sawa na asilimia 52.6 watuhumiwa walitiwa hatiani na kesi 3 sawa na asilimia 15.8 watuhumiwa waliachiwa huru. Aidha, kesi 3 sawa na asilimia 15.8 zilifutwa na Mawakili wa Serikali chini ya Kifungu cha 91 (1) CPA, kesi 2 sawa na asilimia 10.5 kwa watuhumiwa kukiri makosa (Plea Bargaining) na kesi moja (1) sawa na asilimia 5.3 ya kesi zote zilizokwisha ilifutwa kutokana na watuhumiwa kufariki dunia. (Jedwali Na. 11 na Chati Na.4).

**Jedwali 11: Jinsi Kesi Zilivyokamilika - Vikao vya Mahakama Kuu - Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi**

| Aina ya Makosa | Kesi zilizoisha kwa Watuhumiwa kutiwa hatiani | Kesi zilizoisha kwa Watuhumiwa kuachiwa huru | Kesi zilizoondolewa na Mawakili wa Serikali chini ya k/f 91(1) CPA | Kesi zilizofutwa kutokana na watuhumiwa kufariki | Kesi Zilizokamilika kwa Watuhumiwa Kukiri Makosa (Plea Bargaining) |
|---|---|---|---|---|---|
| Dawa za Kulevya | 9 | 3 | 3 | 1 | 2 |
| Nyara za Serikali | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Rushwa, Udanganyifu na Utakasishaji Fedha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ugaidi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Makosa Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **10** | **3** | **3** | **1** | **2** |

**Chati 4: Jinsi Kesi zilivyokamilika kwa Asilimia - Vikao vya Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa Asimilia**




## C. Rufaa na Maombi

### i. Rufaa na Maombi Yaliyoendeshwa

Jumla ya rufaa na maombi 2,148 yalifunguliwa ambapo, maombi na rufaa 1,408 zilikuwepo hadi 31 Disemba, 2022 na maombi na rufaa 740 ziliombwa kati ya Januari na Juni, 2023.

Jumla ya rufaa 1,647 na maombi 501 yalisikilizwa katika Mahakama Kuu ambapo, rufaa 138 na maombi 84 yalikuwa ya Mkurugenzi wa Mashtaka na rufaa 1,509 na maombi 417 yalikuwa dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Aidha, rufaa 521 na maombi 282 yalikuwa yamekamilika ambapo, rufaa 35 na maombi 34 yalikuwa ya Mkurugenzi wa Mashtaka na rufaa 486 na

maombi 248 yalikuwa dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Vilevile, rufaa 1,126 na maombi 219 yanaendelea mahakamani ambapo rufaa 103 na maombi 50 yalikuwa ya Mkurugenzi wa Mashtaka na rufaa 1,023 na maobi 169 yalikuwa dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. (Jedwali Na. 12).

**Jedwali 12: Kesi za Rufaa na Maombi zilizoendeshwa - Mahakama Kuu**

| Aina ya Kesi | Zilizovuka 31 Disemba, 2022 | zilizofunguliwa | Jumla | Zilizokamilika | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|
| Rufaa za DPP | 95 | 43 | **138** | 35 | 103 |
| Rufaa dhidi ya DPP | 1,090 | 419 | **1,509** | 486 | 1,023 |
| Maombi ya DPP | 38 | 46 | **84** | 34 | 50 |
| Maombi dhidi ya DPP | 185 | 232 | **417** | 248 | 169 |
| **Jumla** | **1,408** | **740** | **2,148** | **803** | **1,345** |

### ii. Rufaa na Maombi Yalivyohitimishwa

Jumla ya rufaa 521 na maombi 282 yalikamilika katika Mahakama Kuu sawa na asilimia 37.4 ya rufaa na maombi yote yaliyofunguliwa. Kati ya hizo, rufaa 35 na maombi 34 yalikuwa ni ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 8.6 na rufaa 486 na maombi 248 yalikuwa dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambayo yalikuwa sawa na asilimia 91.4 ya rufaa na maombi yote yaliyofunguliwa. (Jedwali Na. 13).

**Jedwali 13: Jinsi Kesi za Rufaa na Maombi zilivyokamilika - Mahakama Kuu**

| Aina ya Kesi | Zilizokubaliwa | Zilizokataliwa | Zilizotupwa | Zilizokubaliwa kwa Sehemu | Zilizoondolewa na Wahusika | Kusikilizwa Tena (Re-trial) | Kesi Zilizofutwa kutokana na Watuhumiwa Kufariki (Abated) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rufaa za DPP | 12 | 8 | 7 | 0 | 3 | 5 | 0 |
| Rufaa dhidi ya DPP | 230 | 139 | 61 | 21 | 10 | 24 | 1 |
| Maombi ya DPP | 29 | 1 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Maombi dhidi ya DPP | 162 | 26 | 18 | 14 | 9 | 19 | 0 |
| **Jumla** | **433** | **174** | **86** | **35** | **26** | **48** | **1** |

### 4.2.4. Mahakama ya Rufani

#### i. Rufaa na Maombi Yalivyoendeshwa

Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2023 Mahakama ya Rufani iliendesha jumla ya rufaa na maombi 1,457 ambapo, rufaa 167 na maombi 24 yalikuwa ya Mkurugenzi wa Mashtaka na rufaa 1,144 na maombi 122 yalikuwa dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kati hizo, rufaa 111 na maombi saba (7) yalisikilizwa na kumalizika na rufaa 1,200 na maombi 139 yanaendelea kusikilizwa kupitia vikao mbalimbali vya Mahakama ya Rufaa nchini. (Jedwali Na. 14).

**Jedwali 14: Kesi za Rufaa na Maombi zilizoendeshwa - Mahakama ya Rufani**

| Aina ya Kesi | Zilizovuka 31 Disemba, 2022 | Zilizofunguliwa | Jumla | Zilizokamilika | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|
| Rufaa za DPP | 147 | 20 | **167** | 17 | 150 |
| Rufaa dhidi ya DPP | 1,035 | 109 | **1144** | 94 | 1050 |
| Maombi ya DPP | 7 | 17 | **24** | 0 | 24 |
| Maombi dhidi ya DPP | 79 | 43 | **122** | 7 | 115 |
| **Jumla** | **1,268** | **189** | **1,457** | **118** | **1,339** |


#### ii. Rufaa na Maombi Yalivyohitimishwa

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, jumla ya rufaa na maombi 118 katika Mahakama ya Rufani yalikamilika ambapo rufaa 17 zilikuwa za Mkurugenzi wa Mashtaka na rufaa 94 na maombi 7 yalikuwa dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kati ya hayo, rufaa na maombi 61 ambayo ni sawa na asilimia 51.7 yalikubaliwa, rufaa na maombi 28 sawa na asilimia 23.7 yalikataliwa, rufaa na maombi matano (5) sawa na asilimia 4.2 yalitupiliwa mbali. Aidha, rufaa na maombi matano (5) sawa na asilimia 4.2 yalikubaliwa kwa sehemu, rufaa na maombi nane (8) sawa na asilimia 6.8 yaliondolewa na wahusika na rufaa na maombi 10 sawa na asilimia 8.5 yaliamriwa kusikilizwa tena. Wakati huo huo, rufaa moja (1) sawa na asilimia 0.8 dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilifutwa kutokana na watuhumiwa kufariki (abated). (Jedwali Na. 15 na Chati Na. 5).

**Jedwali 15: Jinsi Kesi za Rufaa na Maombi Zilivyokamilika**

| Aina ya Kesi | Zilizokubaliwa | Zilizokataliwa | Zilizotupwa | Zilizokubaliwa kwa Sehemu | Zilizoondolewa na Wahusika | Kurudi Kusikilizwa Tena (Re-trial) | Kesi Zilizofutwa kutokana na Watuhumiwa Kufariki (Abated) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rufaa za DPP | 5 | 2 | 0 | 2 | 4 | 4 | 0 |
| Rufaa dhidi ya DPP | 53 | 25 | 4 | 3 | 2 | 6 | 1 |
| Maombi ya DPP | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Maombi dhidi ya DPP | 3 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **61** | **28** | **5** | **5** | **8** | **10** | **1** |

**Chati 5: Jinsi Kesi za Rufaa na Maombi Zilivyokamilika- Mahakama ya Rufani kwa Asilimia**




### 4.2.5. Faini Zilizotozwa na Mali Zilizotaifishwa

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 washtakiwa mbalimbali waliotiwa hatiani kutokana na kesi za jinai zilizokuwa zinawakabili na walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo, faini na mali mbalimbali zilizohusika katika uharifu kutaifishwa.

Katika kipindi husika (Januari – Juni, 2023) kiasi cha **Shilingi 725,690,880** kililipwa mahakamani kama faini katika kesi 2,836 na kiasi cha **Shilingi 636,413,783.61** zililipwa kama faini na fidia na watuhumiwa waliokili makosa kwa njia ya makubaliano (*Plea bargain*).

Aidha, mali mbalimbali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu ama zilizotumika kutenda uhalifu zilitaifishwa kuwa mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mali hizo ni pamoja na fedha taslim **Shilingi 1,455,698,000** na **Dola za Marekani 2,064,** mifugo (ng’ombe 2,403, mbuzi 19 na kondoo 77), magari 11 na viwanja 7.

**Jedwali 16: Fedha Zilizokusanywa kutokana na Faini katika Makosa Mbalimbali – Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi**

| Aina ya Makosa | Idadi ya Kesi | Jumla ya Faini Zilizolipwa |
|---|---|---|
| Usalama Barabarani | 1,976 | 145,380,321 |
| Nyara za Serikali | 17 | 69,448,294 |
| Maliasili Nyinginezo | 290 | 170,215,000 |
| Dawa za Kulevya | 94 | 39,285,000 |
| Madini | 3 | 24,900,000 |
| Udanganganyifu | 35 | 69,560,000 |
| Utakasishaji Fedha | 1 | 2,000,000 |
| Uhalifu wa Mtandao | 4 | 17,183,000 |
| Usafirishaji wa Binadamu (Human Trafficking) | 1 | 1,000,000 |
| Unyang'anyi wa Kutumia Silaha | 7 | 265,048 |
| Rushwa | 7 | 5,230,000 |
| Kuingia na Kuishi Nchini bila Kibali | 45 | 20,600,000 |
| Makosa Mengineyo | 356 | 160,624,217 |
| **Jumla** | **2,836** | **725,690,880** |

### 4.3. Ukaguzi wa Magereza na Vituo vya Polisi

Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) iliendelea kukagua magereza na vituo vya polisi kwa lengo la kuainisha changamoto za kiutendaji na kiupelelezi na kutoa maelekezo stahiki kutatua changamoto hizo. Katika kipindi husika, jumla ya Magereza 103 na vituo vya Polisi 168 vilikaguliwa na jumla ya mahabusi 1,603 waliachiwa huru kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ushahidi hafifu. Kutokana na kuachia kwa mahabusi waliotajwa kumesaidia kupunguza mlundikano wa mahabusi katika Vituo vya Polisi na Magereza nchini. Taarifa ya Magereza na Vituo vya Polisi vilivyokaguliwa katika kipindi husika ni kama inavyojielekeza katika ***Kiambatisho Na. 2.***

### 4.4. Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi

Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza Progamu ya Kutenganisha Shughuli za Mashtaka na Upelelezi kwa kusogeza huduma za kimashtaka kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Katika kipindi husika, Ofisi ilifungua Ofisi za Wilaya 50 katika mikoa 30 ya Kimashtaka hivyo kufanya jumla ya Ofisi za Mikoa kuwa 30 na Ofisi za Wilaya 94.

Mwezi Aprili, 2023 Ofisi ilifanya kikao kazi kwa lengo la kuboresha Kanzidata ya Waendesha Mashtaka waliopewa kibali cha kuendesha mashtaka na Mkurugenzi

wa Mashtaka. Jumla ya Waendesha **Mashtaka 1,314** hadi sasa wamepewa vibali vya kuendesha mashtaka. Waendesha Mashtaka waliopewa vibali wanatoka katika Wizara, Halmashauri na Taasisi mbalimbali kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 17.

**Jedwali 17: Orodha ya Waendesha Mashtaka Ki-Taasisi/Ofisi na Mikoa**

| Sehemu A | | | | Sehemu B | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Waendesha Mashtaka Kitaasisi/Ofisi | | | | Idadi ya Waendesha Mashtaka Kimkoa | | |
| Na. | Jina la Taasisi/Ofisi | Idadi Waendesha Mashtaka | | Na. | Jina la Mkoa | Idadi Waendesha Mashtaka |
| 1 | Jeshi la Polisi | 498 | | 1 | Wizara na Makao Makuu ya Ofisi/Taasisi mbalimbali | 885 |
| 2 | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa | 207 | | 2 | Morogoro | 39 |
| 3 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 89 | | 3 | Mara | 36 |
| 4 | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) | 78 | | 4 | Mtwara | 22 |
| 5 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 54 | | 5 | Mwanza | 28 |
| 6 | Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) | 47 | | 6 | Kagera | 21 |
| 7 | Uhamiaji | 170 | | 7 | Kilimanjaro | 21 |
| 8 | Wakala wa Vipimo | 29 | | 8 | Dodoma | 13 |
| 9 | Mamlaka ya Mapato Tanzania | 30 | | 9 | Tanga | 23 |
| 10 | Jeshi la Zimamoto | 28 | | 10 | Arusha | 16 |
| 11 | Wizara ya Katiba na Sheria | 25 | | 11 | Manyara | 20 |
| 12 | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) | 13 | | 12 | Ruvuma | 16 |
| 13 | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 3 | | 14 | Lindi | 23 |
| 14 | Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA-CHEMIST) | 4 | | 15 | Pwani | 20 |
| 15 | Wataalamu wa maandishi na alama za vidole | 10 | | 16 | Iringa | 11 |
| 16 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 12 | | 17 | Geita | 12 |
| 17 | Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya | 10 | | 18 | Songwe | 10 |
| 18 | Halmashauri ya Jiji | 4 | | 19 | Mbeya | 9 |
| 19 | Halmashauri ya Manispaa | 4 | | 20 | Kigoma | 25 |
| 20 | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) | 1 | | 21 | Rukwa | 10 |
| 21 | Tume ya Uchaguzi | 1 | | 22 | Dsm | 16 |
| 22 | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | 4 | | 23 | Singida | 6 |
| 23 | Wataalamu wa makosa ya mtandao | 29 | | 24 | Temeke | 7 |
| 24 | Wataalamu wa milipuko | 7 | | 25 | Tabora | 10 |
| 25 | Wataalamu wa picha | 183 | | 26 | Njombe | 6 |
| 26 | Bodi ya Wakandarasi | 1 | | 27 | Simiyu | 5 |
| 27 | Halamashauri ya Wilaya | 2 | | 28 | Katavi | 2 |
| | | | | 29 | Shinyanga | 2 |
| | | | | | | |
| | **Jumla** | **1,314** | | | **Jumla** | **1,314** |

### 4.5. Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika Makosa ya Jinai

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 OTM imetekeleza jukumu hili kama ifuatavyo;

#### 4.5.1. Ushirikiano wa kitaifa

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa haki jinai katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji kama ifuatavyo;

i. Mwezi Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) zimefanya ukaguzi katika Ofisi za Mikoa za Taasisi hizo. Lengo la ukaguzi huo, pamoja na mambo mengine ilikuwa ni kufanya tathmini ya utekelezwaji wa majukumu ya Ofisi za Mikoa na uzingatiaji wa utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika hatua ya upelelezi na ufunguaji wa mashtaka;

ii. Mwezi Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliandaa kikao kazi cha kuandaa rasimu sifuri (Zero Draft) ya Mwongozo wa Kiutendaji wa Ushughulikiaji wa Kesi zinazohusisha Mifugo inayoingizwa katika maeneo yaliyohifadhiwa. Mwongozo huu unalenga kupunguza/kama si kumaliza changamoto zinazotokana na kesi za mifugo inayoingia hifadhini. Changamoto hizi zimepelekea kuwepo na ugumu wa ushughulikiaji na uendeshaji wa kesi hizo kiasi cha kusababisha Serikali kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wafugaji na kuingia gharama za kufidia mifugo yao. Mwongozo huu utasaidia kuepusha malalamiko ya wananchi na kusaidia Serikali kuepuka gharama kubwa za kulipa fidia;

iii. Mwezi Aprili, 2023 OTM kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifanya kikao kazi cha pamoja kati ya waendesha mashtaka na wachunguzi cha kupitia majalada 24 ya Makosa Makubwa ya Rushwa, Udanganyifu na Uhujumu Uchumi. Lengo la mapitio hayo lilikuwa ni kuharakisha ushughulikiaji wa majalada yaliyokaa muda mrefu bila kutolewa maamuzi. Majalada haya

yalikamilishwa kwa kuandaliwa hati za mashtaka ambazo zimesajiliwa katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Rushwa;

iv. Mwezi Februari, 2023 Ofisi ya Tifa ya Mashtaka, ilishiriki katika Madhimisho ya Matumizi Salama ya Mtandao *"Safer Internet Day, 2023"* yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) - Dodoma. Katika maadhimisho haya washiriki walipata fursa kujengewa uwezo juu ya matumizi salama ya mtandao. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipata fursa ya kutoa maada katika maadhimisho;

v. Mwezi Mei, 2023 OTM ilianda na kuzindua Mwongozo wa Kusimamia Ushirikiano wa Taasisi katika Kupeleleza na Kuendesha Mashtaka ya Utakatishaji Fedha Haramu, Ugaidi, na Ufadhili wa Ugaidi (Inter-Agency Cooperation, Collaboration and Cordination in the Investigation and Prosecutions of Money Laundering, Terrorism and Terrorsim Financing). Uandaaji wa Mwongozo huu ulishirikisha taasisi mbalimbali zinazojishughulisha na makossa tajwa ambazo ni Ofisi ya Rais, TAKUKURU, Benki Kuu, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, BRELA, RITA, Kitengo cha Kuzuia Utakatishaji Fedha Haramu (FIU), Msajili wa Taasisi Zisizo za Kiserikali, Msajili wa Jumuiya na Balaza la Usimamimizi wa Taasisi Zisizo za Kiserikali (NACONGO). Mwongozo huu umelenga pamoja na mambo mengine kuboresha mifumo ya kupeana taarifa (Information Sharing), Usimamizi wa Upelelezi chini ya OTM, Ujumuishaji wa Jamii katika kuzuia makossa tajwa hapo juu na ujengaji wa uwezo wa watendaji katika taasisi;

vi. Vile vile, OTM Mwezi Februari, 2023 iliendelea na mchakato wa kuandaa Rasimu ya Muongozo wa Kushughulikia Makosa ya Mtandao kwa Waendesha Mashtaka na Wapelelezi. Rasimu ya Awali ya Muongozo imekamilika na imewasilishwa kwa Menejimenti ya OTM na kupata ridhaa ya kupelekwa kwa wadau kwa nia ya kupata maoni na hatimaye kuzinduliwa rasmi kwa ajili ya kuanza kutumika. Maandalizi haya ya rasimu yalifanyika kwa kushirikiana na Mawakili wa Serikali wa

OTM pamoja na Maafisa Wachunguzi na Wapelelezi wa Makosa ya Mtandao kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mkosa ya Jinai nchini. Lengo la Muongozo huu ni kurahisisha utendaji kazi kwa Mawakili wa Serikali, Waendesha Mashtaka na Wapelelezi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

vii. Mwezi Mei, 2023 OTM ilishiriki Kikao cha 12 cha kawaida cha Kamati ya Kitaifa ya Usalama wa Usafiri Majini (NMSC) katika ukumbi wa mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, lengo la kikao hicho ilikuwa ni mwendelezo wa kikao cha 11 pamoja na kwenda kutembelea eneo la kusafirishia abiria wanokwenda Zanzibar. Katika kikao hicho wajumbe waliazimia kuwa eneo la kusafiria abiria lililotembelewe litembelewe tena kabla kandarasi hajakabidhi kazi ili kuona ubora na mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi ujulishwe Uongozi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa barua. Kikao kitakachofuata kitafanyika Zanzibar kwa mujibu wa makubaliano na mapendekezo ya wajumbe;

viii. Machi, 2023 OTM ilishiriki Warsha ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa "*Financial Action Task force"* (FATF) Jijini Dar es salaam. Lengo la warsha lilikuwa kupata maelezo ya jitihada na weledi wa kutekeleza kuondoa mapungufu yaliyojitokeza kwenye taarifa ya tathimini iliyotolewa Juni 2021 kuhusu mapungufu ya sheria na utekelezaji wake katika kuzuia utakatishaji fedha wa fedha haramu na kuzuia ugaidi na ufadhili wa ugaidi. OTM iliwasilisha mada ya changamoto katika upelelezi na uendeshji kwa mashtaka ya ugaidi pamoja na masuala ya "*cyto currence na bit coin"*;

ix. Mei, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki kikao cha Mawakili Wasio na Mipaka (Lawyers without Borders/DPPs Round Table) ambacho kiliwahusisha Wakurugenzi wa Mashtaka kutoka Kenya, Uganda, Tanzania na Zanzibar. Kikao kilifanyika Zanzibar na lengo lilikuwa ni kuongeza ushirikiano ili kuhakikisha kuwa upelelezi na uendeshaji wa kesi zinazohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu unaimarishwa ili ufanisi katika kesi hizi unapatikana. Aidha, kikao kiliazimia kuwapa

ushirikiano mawakili wasio na mipaka kwa kuwajengea uwezo Wapelelezi, Waendesha Mashtaka na Mahakimu;

x. Mwezi Mei, 2023 OTM ilishiriki warsha ya muendelezo wa utekelezaji wa mpango kazi wa "*Financial Action Task force*" (FATF) Dar es Salaam, lengo la warsha ilikuwa kupitia Sheria ya Kuzuia Ugaidi Tanzania ili kupata uelewa wa pamoja juu ya makosa ya ugaidi chini ya Sheria ya Tanzania, uzoefu wa upelelezi na uendeshaji wa mashtaka yanayohusu ugaidi na changamoto za kisheria zilizowahi kujitokeza. Malengo mengine ya warsha yalikuwa ni kuwa na uelewa juu ufadhili wa ugaidi na kuelewa vigezo vilivyowekwa kisheria ili kuweza kumshauri Waziri mwenye dhamana juu ya hatua za kisheria za kuchukua pindi mtu/taasisi kupitia shughuli za kiuchumi inapobainika kufadhili ugaidi au vitendo vya kigaidi. Aidha, lengo lilikuwa ni kubadilishana uzoefu juu ya uelewa wa fedha za kidigitali (Crypto Currency and Bitcoin) na changamoto za kisheria zilizopo juu ya udhibiti wa miamala ya aina hii kwa Sheria za Tanzania na mianya iliyopo inayoweza kupelekea ufadhili wa ugaidi usioweza kugundulika kwa urahisi;

xi. Mei, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki kikao kazi na maofisa upelelezi wa Jeshi la Polisi ili kujadili utekelezaji wa maombi 18 ya kukusanya ushahidi yaliyopokelewa kutoka nchi mbalimbali. Kati ya maombi hayo, maombi 13 yaliwasilishwa kukusanya ushahidi kwenye nchi mbalimbali, maombi 4 tuliyopokea ya kukamata watuhumiwa waliodaiwa kukimbilia Tanzania na maombi 5 tuliyatuma kukamata watuhumiwa walioko nchi za nje. Katika kikao hicho tulibaini mafanikio katika baadhi ya maombi hayo na uwepo wa mkwamo wa utekelezaji katika baadhi ya maombi kunakotokana na baadhi ya nchi, mathalani Kenya na Uganda kutotoa ushirikiano wa kutosha katika kushughulikia maombi hayo. Vile vile, kumekuwepo changamoto ya kisheria kuhusiana na maombi yanayowasilishwa pale yanapohusisha ushahidi unaopatikana Tanzania Zanzibar kwa kigezo cha Mamlaka inayoweza kupokea na kushughulikia maombi hayo;

xii. Mwezi Juni, 2023 OTM ilishiriki kikao kazi cha kupitia majalada yote ya kesi za dawa za kulevya zilizoko mahakamani mkoa wa Arusha ili kubaini changamoto za kiupelelezi na mashtaka kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi wa kisheria. Zoezi lilihusisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Mawakili wa Serikali kutoka Makao Makuu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wale wa Mkoa wa Arusha. Katika zoezi hili ilibainika kuwa changamoto ilikuwa ni kutozingatia taratibu za kisheria wakati wa hatua za ukamataji watuhumiwa (Arrest), ukamataji wa dawa (search and seizure), utunzaji wa vielelezo na utunzaji wa mnyororo wa makabidhiano ya vielelezo. Changamoto nyingine zilijumuisha ucheleweshaji wa majibu ya uchunguzi vielelezo kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na kutozingatiwa utaratibu wa kuharibu vielelezo (disposal of drugs). Kutokana na changamoto hizo kulifanyika mafunzo ili kuondoa/kupunguza changamoto hizo yaliyoongozwa na Kamisha wa Sheria kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya yaliyowahusisha Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, Wakuu wa Upelelezi kutoka wilaya zote za Mkoa wa Arusha na baadhi wa wapelelezi mkoani humo; na

xiii. Mei, 2023 OTM ilishiriki kikao cha kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kudhibiti Biashara ya Usafirishaji Binadamu 2021-2024 (*National Anti-Trafficking in Persons Plan of Action 2021-2024*) Jijini Dodoma. Kikao kazi kiliandaliwa na Sekretarieti ya Kudhibiti Biashara ya Usafirishaji Binadamu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM). Lengo la kikao ilikuwa kufanya tathmini ya maazimio, malengo na utekelezaji kwa muda uliopangwa wa maazimio ya kupambana na Biashara ya Usafirishaji Binadamu. Mkakati uliojikita katika kuzuia (*Prevention*), kulinda (protection), prosecution (mashtaka), ushirikishaji wadau (partnership) na masuala mtambuka (Crosscutting issues). Baada ya tathmini ilibainika kuwa Mpango Kazi wa Taifa ulionyesha mafanikio katika maeneo yaliyowekewa maazimio na malengo, mathalani, kupitishwa kwa Sheria ya Kudhibiti Biashara ya Usafirishaji Binadamu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar na

Uanzishwaji wa Nyumba Salama (*Safe Houses*) kwa ajili ya wahanga wa matukio. Changamoto zilizobainishwa ni kwa baadhi ya wadau kutotekeleza Mpango Kazi kama ulivyo hasa katika eneo la utunzaji wa kumbukumbu sahihi (*data*) za matukio na jinsi yalivyofanyiwa kazi kunakopelekea kutokuwa na taarifa zinazoshabihiana baina ya wadau. Kikao kiliazimia kila mdau kutekeleza maazimio na malengo ili kuweza kufikia malengo tarajiwa kabla ya mwisho wa Mpango Kazi Juni, 2024.

### 4.5.2. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023, OTM iliendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha ushirikano wa kikanda na kimataifa kwa kushiriki katika mikutano na kongamano za kimataifa kuhusu masuala mbalimbali ya kitaalamu na mapambano dhidi ya uhalifu kama ifutavyo: -

i. Mwezi April, 2023 Ofisi imeshiriki katika kikao kazi cha kuandaa majumuisho ya maamuzi ya Mahakama katika kesi za wanyamapori (Developing a Wildilife Case Digest) kwa nchi wanachama wa Umoja wa Waendesha Mashtaka wa Nchi za Afrika Mashariki (Eastern Africa Association of Prosecutors). Kikao hiki kilifanyika Nairobi Kenya na kuwakutanisha pamoja maafisa viunganishi (focal persons) kutoka Nchi Wanachama wa Umoja wa Waendesha Mashtaka. Lengo kuu la kikao hiki lilikuwa ni kuandaa kuandaa majumuisho ya maamuzi ya Mahakama katika kesi za wanyamapori ili kupata uzoefu kutoka nchi wanachama pamoja na kufanya mapitio na kurekebisha Mpango Mkakati wa Umoja huu;

ii. Mwezi Mei, 2023 Ofisi ilishiriki Kikao cha 32 cha Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Kuzia Uhalifu na Hakijinai kilichofanyika Vienna Nchini Austria. Kikao hicho kiliandaliwa na Nchi ya Ghana ikiwa ni Nchi Mwenyekiti wa Kamisheni hiyo kwa upande wa Afrika. Lengo la kikao lilikuwa ni kujadili masuala yanayohusu namana bora ya kuzuia uhalifu na mfumo mzima wa Haki Jinai kwa nchi wanachama. Kupitia kikao hicho, nchi wanachama ziliweza kubadilishana uzoefu wa mbinu mbalimbali za kupambana na uhalifu, umuhimu wa uzingatiaji wa Haki za Binadamu katika utekelezaji wa majukumu, umuhimu wa ushirikiano

baina ya nchi wanachama na taasisi za Kimatafa na mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia;

iii. Mwezi Juni, 2023 Ofisi ilishiriki warsha ya Kuandaa Mkakati na Mafunzo ya Nyenzo za Ufatiliaji wa Kesi Mahakamani (*EAAP Strategic Plan and Training on Application on the Court Case Tracking Tool)* iliyofanyika, Kigali Rwanda. Warsha hiyo iliandaliwa na Sekretarieti ya Umoja wa Afrika wa Waendesha Mashtaka wa Afrika Mashariki (*Eastern Africa Association of Prosecutors Secretariet*). Lengo la warsha hiyo ilikuwa ni kuandaa na kupitia Mpango Mkakati wa Miaka Mitano EAAP, Kupitia jarida la mashauri mbalimbali na mfumo wa ukusanyaji na utunzaji taarifa. Kupitia warsha hiyo, washiriki walijadili hoja mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa taarifa, mashauri ya wanayama pori, na kupitisha Mapango Mkakati wa miaka mitano;

iv. June, 2023 Mawakili wa Serikali 15 kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka walishiriki mafunzo yaliyoandaliwa na *"International Computer Hacking and Intellectual Property (ICHIP)"*. Mafunzo yalilenga kujajadili Sheria ya Makosa ya Mtandao na mapungufu yaliyopo. Aidha, masuala ya "*cryptocurrency"*, ukusanyaji na uwasilishaji wa ushahidi wa kielektoniki, ushirikiano wa kimataifa na jinsi ya kufundisha Waendesha Mashtaka. Pia, mbinu za kufundisha watu wazima, jinsi ya kutengeneza rasilimali kwaajili ya kuwafikia Waendesha Mashtaka na jinsi ya kupanga na kukamilisha maelengo yalitolewa mafunzo;

v. Mwezi Mei, 2023 OTM ilishiriki ziara ya mafunzo iliyoandaliwa na "*International Computer Hacking and Intellectual Property"*. Ziara hii ilifanyika nchini Marekani katika Jimbo la North Carolina- Greensboro na Jimbo la Washington DC. Ziara ilijumuisha Majaji, Waendesha Mashtaka na Wapelezi kutoka badhi ya nchi za afrika. Lengo la ziara hii lilikua ni kukutanisha Majaji, Waendesha Mashtaka na Wapelezi kutoka katika baadhi ya nchi za afrika kukutana na Majaji, Waendesha Mashtaka na Wapelezi wa Nchi ya Marekani kwa nia ya kuelimishana, kubadilishana mawazo pamoja na kujadili changamoto mbalimbali wanazokutana nazo katika kupambana na uhalifu unaofanyika kwa njia

ya mtandao. Ziara hii pia ililenga kudumisha mahusiano ya kiutendaji kati ya nchi na nchi hasa katika masuala ya ushirikiano wa kimataifa;

vi. Mwezi June, 2023 Ofisi ya Taifa mashtaka ilishiriki Kongamanol a Kikanda lililofanyika nchini Misri kuhusiana na nafasi ya ushahidi wa kidigitali katika kupambana na makosa ya kupangwa na yanayovuka mipaka. Kongamano lililoandaliwa na "*International Organization for Migration (IOM)"* wakishirikiana na Ofisi ya Mashtaka Misri. Lengo la kongamani hili ilikuwa ni kutengeneza jukwaa la kikanda la kubadilishana ujuzi na kutafuta njia bora ya kukabiliana na uhalifu wa mtandao. Aidha, Kongamano lililenga pia kujenga uelewa juu ushahidi wa kidigitali unaotumika katika usafirishaji haramu wa binadamu, kuainisha na kutambua mikataba na sheria mbalimbali na kimataifa na kitaifa zinazotumika katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na makosa ya imtansdao. Vile vile, usfirishaji haramu wa binadamu, makosa ya kimtandao pamoja na hali halisi ya mtandao uliopo wa wahalifu wa makosa ya kupangwa elimu ilitolewa. Pia, kuangalia hali halisi iliyopo sasa kuhusiana na kutafuta namna bora ya kukuza mahusiano na ushirikiano katika ubadilishanaji wa taarifa muhimu za uhalifu katika eneo hili ulijadiliwa;

vii. Juni, 2023 OTM ilishiriki warsha iliyofanyikia Jijini Dar es Salaam Tanzania katika kuimarisha mbinu ya kubadilishana ushahidi na wahalifu Kimataifa baina ya nchi tatu (3) ambazo ni Malawi, Musumbiji na Tanzania iliyoandaliwa na *"The International Institute of Justice and Rule of Law (IIJ)*" wakishirikiana na Serikali ya Marekani. Lengo la warsha hii ni kuainisha mapungufu yaliyopo kwenye sheria zetu yanayopelekea kuleta mkwamo katika utekelezaji wa kesi za jinai kimataifa. Pia, kuongeza uelewa juu ya matumizi ya sheria kitaifa katika kuendana na kimataifa katika masuala ya kusaidiana kupatikana ushahidi na kurudisha wahalifu toka nchi nyingine yalijadiliwa. Vile vile, washiriki walijadili mapendekezo ya namna nzuri kitaifa na kimataifa katika kusaidiana kupatikana ushahidi na urudishwaji wa wahalifu kwenye nchi alikotendea tukio. Katika warsha hii washiriki waliweza kujifunza namna nzuri ya kuendeleza mashirikiano ya kimataifa katika

kusaidiana kupatikana kwa ushahidi pamoja na kurudisha watuhumiwa waliokimbilia nchi nyingine ikwemo kusaini mikataba ya ushirikiano kimataifa ya namna ya kusaidiana kupatikana ushahidi na watuhumiwa;

viii. Mwezi Juni, 2023 OTM ilishiriki katika Warsha ya Kitaifa kuhusu Kuzingatiaji Masharti ya Mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Bahari Duniani hususan masuala ya usalama kwenye sheria za nchi iliyofanyikia Dar es Salaam Tanzania. Warsha hii iliendeshwa na wawakilishi toka Shirika la Bahari Duniani *(“International Marine Organization”).* Washiriki wengine wa Warsha hii, walikuwa Wakala wa Meli Tanzania (TASC), Mamlaka ya Kuthibiti Dawa za Kulevya (DCEA), Mamlaka ya Bandari Tanzania (PTA), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AGC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Uhamiaji na Polisi Wanamaji. Lengo la Warsha hii lilikuwa kujifunza majukumu na wajibu wa nchi zilizopo Ukanda wa Bahari (“*Costal State Responsibilities*”) na wajibu wa Vyombo vya Ulinzi wa Bandari (“Port Security Rensponsibilities)”. Aidha, washiriki walifundishwa umhimu wa kuitungia au kuichukua na kuifanya Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia kuweza kuingizwa kwenye sheria za Tanzania ambao ni “*International Convention for Safety of Life at Sea* (SOLAS) Chapter XI-2”. Washiriki walijifunza namna ya utendekaji wa makosa ya majini na namna bora ya kupambana na uhalifu wa majini;

ix. Mwezi Mei, 2023 OTM walihudhuria warsha iliyofanyikia Mjini Gaborone nchini Botswana iliyoandaliwa na “*Internatonal law Enforcement Academy (ILEA)*” kwa kushirikiana na Ubalozi wa Marekani. Washiriki wa warsha hili walitoka nchi saba (7) ambazo ni Zambia, Tanzania, Malawi, Lesotho, Togo, Republic of Congo, na Botswana. Lengo la warsha hii ilikuwa ni kubadilishana uzoefu na namna bora ya kupambana na makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu. Aidha, washiriki walijifunza namna bora ya kuandaa sera na kuboresha sheria kwa lengo la kuanzia NGOs na vituo kwa ajili ya waathirika wa usafirishwaji haramu wa binadamu pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau wa usimamizi na utekelezji wa sharia;

x. June 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki warsha nchini Zambia iliyoandaliwa na Umoja wa Ulaya (*European Union*) kupitia mradi wa *“Anti-Money Laundering and Counter Financing of Terrorism in Eastern, Southern, Central Africa and Yemen”* ambao walifadhiri warsha. Warsha hii ilihusu *“Asset Recovery and Confiscation”*. Warsha hii ilihudhuriwa na washiriki 89 kutoka nchi 23 ambazo ni Zambia, Tanzania, Uganda, Kenya, Angola, Botswana, Malawi, Madagascar, Mauritus, Monzambique, South Africa, South Sudan, Zimbabwe, Seychelles, Burundi, Eswatin, Eritrea, Ethiopia, Namibia, Rwanda, Somalia, Djibout na Yemen. Lengo la warsha hii ni kuongeza uelewa faida/manufaa ya kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia za uhalifu hususani katika kuzuia uhalifu, kuongeza ufanisi katika urejeshaji na utaifishaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu. Aidha, kusaidia uelewa wa utamaduni wa uchunguzi wa kifedha (Financial Investigation) na uwezo wa washiriki wa mafunzo katika kupanga na kutekeleza uchunguzi wa kifedha, kutambua, kutafuta, kushikilia kwa muda na kutaifisha mali au mazalia ya uhalifu. Washirki wote wa warsha waliazimia kudumisha ushirikiano ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali kwa njia isiyo rasmi zitakazowezesha kuharakisha mapambano dhidi ya fedha haramu pamoja na mali zilizopatikana kwa njia isiyo halali hususani zinazovuka mipaka ya nchi;

xi. Mwezi Januari, 2023 OTM ilishiriki katika Mkutano wa Awamu ya Nne (4) wa Kamati ya Muda ya Majadiliano ya Kuanzishwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Kukabiliana na Matumizi ya Teknolojia Habari kwa Njia ya Jinai huko Nchini Marekani. Mkutano huu ulihudhuriwa na washiriki kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Jeshi la Polisi Tanzania pamoja na Mamlaka ya Ununuzi na Ugavi Tanzania (PPRA). Katika Mkutano huo yalifanywa majadiliano ya kina katika maeneo matatu ambayo ni uhalifu (criminalization), hatua za kiutaratibu na utekelezaji wa sheria (procedural measures and law enforcement) na vifungu vya jumla (general provison). Maeneo haya yalijadiliwa katika

mizunguko miwili, mzunguko wa kwanza wa majadiliano ulifanyika ili kupata maoni ya jumla kutoka nchi wanachama, mashirika yasio ya kiserikali, wasomi na wadau mbalimbali wa TEHAMA kwa nia ya kubaini maeneo yanayokubalika na nchi wanachama kuwa yaingizwe katika mkataba husika. Pia, mkutano ulibaini maeneo ambayo yameonekana kuwa na mgawanyiko mkubwa kati ya nchi wanachama kuwa yaingizwe au yasiingizwe katika mkataba huu. Kwa maeneo ambayo yalikubalika kuingizwa katika mkataba yalijadiliwa na kamati na kwa maeneo yaliyoonekana kuwa na mgawanyiko wa maoni kutoka kwa nchi wanachama yalipelekwa kujadiliwa kwenye *“Co-facilitated Negotiations Group”* kwa majadiliano na ufafanuzi zaidi na matokeo kurudishwa kwenye kamati kwa maamuzi;

xii. Mwezi Februari, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilikutana na kufanya majadiliano na wawakilishi wa “*International Computer Hacking and Interllectual Propaerty (ICHIP)”* ambao ni Bw. Ramaswamy Anand na Bw. Temesgen Lapisa na kufanya nao majadiliano ya jinsi gani Serikali ya Marekani kupitia (ICHIP) itasaidia kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali pamoja na Wapelelezi. Aidha, lengo lilikuwa ni kuwapatia mafunzo ya pamoja watendaji kuhusiana na makosa ya mtandao, jinsi yanavyotendeka, jinsi ya kuyaendesha mahakamani na kuwasilisha ushahidi wa kielektroniki mahakamani;

xiii. Mwezi Aprili, 2023 OTM ilishiriki “*1st Interpole Webinar”* uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huu uliandaliwa na “*Interpole” kwania* ya kutoa uelewa juu ya Mkataba wa Kimataifa unaohusu Kupambanana na Matumizi ya Teknolojia ya Habari kwa Njia ya Jinai. “*Interpole”* iko tayari kusaidia nchi wanchama katika kutoa msaada wa kiufundi pamoja na kujengea uwezo watendaji wanahuskika katika kupambana na uhalifu wa kimtandao;

xiv. Mwezi Mei, 2023 OTM ilishiriki warsha iliyofanyika Sheshamane, nchini Ethiopia iliyokuwa inahusiana na kujengea uwezo wa kupeleleza, kusimamia na kuendesha mashauri ya ugaidi na mashauri ya ukatili yakiwemo ya ukatili kijinsia. Warsha hii iliandaliwa na Shirika la

Kimataifa liitwalo *“Intergoernment Authority on Development (IGAD) center of Excellence for Preventing and Countering Violent Extremism (ICEPCVE)* kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali liitwalo *Sweden Sverige*. Lengo la warsha hii ni kubadilishana uzoefu wa namna wa kupeleleza na kuendesha kesi za ugaidi mahakamani pamoja na kutoa mapendekezo ya namna ya kuongeza ufanisi katika upelelezi na uendeshaji wa mashtaka ya makossa ya ugaidi na mengine yote yenye ukatili mkubwa. Maazimio yaliyofikiwa katika warsha hii ni nchi zote kuimarisha ushirikiano na mawasiliano mazuri ili kutokwamisha hatua za upelelezi, uendeshaji na usikilizaji wa mashauri haya;

xv. Mwezi April, 2023 OTM ilishiriki Kongamano lililofanyika nchini Madagascar kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la *United Nation on Drudgs and Crimes – (UNODC)*. Washiriki walitoka nchi za Comoros, Kenya, Madagascar, Mauritius, Musumbiji, Seychelles, Somalia, Nigeria, Togo, Benin, Ivory Coast, Ghana and Tanzania. Lengo la Warsha ni kujadili makosa yanayotokea baharini na kuwajengea uwezo waendesha mashtaka kutoka nchi za Ukanda wa Baharini namna ya kupeleleza, kukamata, kuendesha kesi zinazohusiana na makosa ya bahariani;

xvi. June, 2023 OTM ilishiriki katika zoezi la kumrejesha mtuhumiwa OLGA D/o KTYSTOP kutoka Bulgaria raia wa Ukraine ambaye ni mtuhumiwa kwenye kesi Na. Eco 15/2023 ya usafirishaji haramu wa Nyara za Selikari ambao ni kobe 116 waliopelekwa nchini Thailand. Zoezi hili lilikamilika na kusomewa hati ya mashtaka katika mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu;

xvii. Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilishiriki Warsha Jijini Nairobi nchini Kenya lililoandaliwa na *“Internation Institute of Justice and rule of Law”* iliyohusiana na kuwajengea uwezo washiriki namna ya kupambana na ugaidi. Lengo la warsha ilikuwa ni kuongeza uelewa kwa washiriki namna ya kushugulikia mapungufu kwa ngazi ya taifa katika kupambana na ugaidi, kubadilishana uzoefu baina ya washiriki

toka nchi tofauti. Maazimio yaliyofikiwa katika warsha ni kuendeleza na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa dhidi ya kupambana na vitendo vya ugaidi;

xviii. Mwezi Mei, 2023 OTM ilishiriki Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa juu ya majadiliano ya Mkataba Wa Kimataifa dhidi ya Uhalifu wa Mtandao (International Convetion on Countering the List of Information and Communications Technologies for Criminal Purposes) uliofanyikia Viena Austria. Lengo la Mkutano ilikuwa ni mwendelezo wa majadiliano katika eneo la ushirikiano wa kimataifa (International Cooperation), usaidizi wa kiufundi (Technical Asisstance), hatua za kuzuia (Prevention Measures), taratibu za utekelezaji (Mechanisms of Implementations), Masharti ya mwisho (Final Provisions) na Utangulizi (Preamble). Sambamba na mkutano huu vilifanyika vikao vya wataalamu ulihusisha (Co-facilitated Informal Consultant Actions) kujadili maeneo ambayo hayakufikia makubaliano ili yaweze kujadiliwa kwa kina na kufikiwa makubaliano yenye tija; na

xix. Machi, 2023 OTM ilishiriki Kongamano nchini Mauritius cha Wakuu wa *"Asset Recovery Agency".* Lengo la Kongamano ilikuwa ni kukutanisha pamoja wakuu wa taasisi (za nchi za Kusini mwa Africa) zinazosimamia masuala ya utaifishaji wa mali zinazohusiana na uhalifu kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya pamoja katka kuimarisha mifumo ya utaifshaji wa mali zinazohusiana na uhalifu pamoja na usimamizi madhubuti wa mali hizo. Aidha, Kongamano lililenga kuongeza ushirikiano wa kimataifa katika kusaidia kurejesha mazalia ya uhalifu pamoja na kutekeleza amri za kutaifisha zilizotolewa na Mahakama toka nchi ya nje.

### 4.6. Kuunganisha Mifumo ya Kukusanya, Kuchakata na Kutunza Taarifa za Masuala ya Uendeshaji wa Mashtaka katika Taasisi za Haki Jinai

Katika kipindi husika, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutumia Mfumo wa Kukusanya, Kuchakata na Kutunza Taarifa za Masuala ya Uendeshaji wa Mashtaka (NPS-CMIS) kwa matumizi ya Ofisi. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023 OTM imeendelea kushirikiana na Wadau wa Haki

Jinai ili kuifanya mifumo ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa na takwimu kusomana. OTM kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao imeweza kuunganisha Mfumo NPS-CMIS na Mfumo wa Jeshi la Polisi na TAKUKURU na kwa sasa Mfumo uliounganishwa umeanza kutumika kwa baadhi ya ofisi za taasisi husika. Kukamilika kwa zoezi hili kutaboresha na kurahisisha upatikana wa taarifa katika mnyororo mzima wa Haki Jinai.

## 4.7. Kuimarisha Huduma za Mashtaka

### 4.7.1. Maendeleo ya Rasilimali Watu

Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2023 hadi Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kutekeleza masuala mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya rasilimali watu. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imeendelea na taratibu za kujaza nafasi zilizowazi. Katika kipindi husika Ofisi imeajiri **Watumishi 315** ambapo **Mawakili wa Serikali ni 281** na **Makatibu sharia ni 34**. Hivyo basi, hadi Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ina jumla ya **watumishi 915** kati ya hao, Mawakili wa **Serikali ni 669**, **Makatibu Sheria ni 84** na **kada nyingine ni 162**. Hata hivyo, licha ya kuajiri watumishi hao, kwa mujibu wa muundo bado kuna upungufu wa **watumishi 4,810.**

### 4.7.2. Kushughulikia Malalamiko Yaliyowasilishwa katika Ofisi

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeshughulikia jumla ya barua za malalamiko 472 kati ya hizo, barua 441 sawa na asilimia 93.4 ya malalamiko yote zilishugulikiwa na kutolewa uamuzi na barua za malalamiko 31 sawa na asilimia 6.6 zinaendelea kufanyiwa kazi.

Tathmini inaonesha malalamiko dhidi ya Jeshi la Polisi yamekuwa mengi ukilinganisha na vyombo vingine vya Haki Jinai. Malalamiko 353 sawa na asilimia 74.8 ya malalamiko yote yalielekezwa upande wa Jeshi la Polisi pekee. Pamoja na malalamiko mengi kuelekezwa Jeshi la Polisi, hata hivyo, malamiko 325 kati ya 353 yaliyoelekezwa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 92.1 yamefanyiwa kazi. (Jedwali Na. 18).

**Jedwali 18: Taarifa ya Barua za Malalamiko**

| Aina ya Malalamiko | Zilizovuka | Zilizopokelewa | Jumla | Zilizofanyiwa Kazi | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|
| Dhidi ya Polisi | 0 | 353 | **353** | 325 | 28 |
| Dhidi ya Mawakili wa serikali | 1 | 1 | **2** | 2 | 0 |
| Dhidi ya Mahakama | 0 | 37 | **37** | 37 | 0 |
| Dhidi ya TAKUKURU | 0 | 8 | **8** | 7 | 1 |
| Dhidi ya Uhamiaji | 2 | 1 | **3** | 2 | 1 |
| Dhidi ya Magereza | 0 | 14 | **14** | 14 | 0 |
| Dhidi ya OTM | 0 | 34 | **34** | 34 | 0 |
| Dhidi ya Taasisi Nyingine | 0 | 21 | **21** | 20 | 1 |
| **Jumla** | **3** | **469** | **472** | **441** | **31** |

#### 4.7.3. Uratibu na Usimamizi wa Jukwaa la Haki Jinai

Katika kipindi husika (Januari – Juni, 2023) OTM iliendelea na zoezi la kuratibu na kusimamia Jukwaa la Haki Jinai nchini. Katika kipindi hiki Ofisi ilifanikiwa kufanya Kikao cha Sekretarieti ya Jukwaaa la Haki Jinai Taifa kinachojumuisha wajumbe kutoka Taasisi mbalimbali za haki jinai, ambacho kilifanyika tarehe 21 Juni, 2023 hadi 22 Juni, 2023 kwa ajili ya maandalizi Kikao cha Jukwaa la Haki Jinai Taifa. Kikao cha Jukwaa la Haki Jinai Taifa kilipangwa kufanyika mwezi Juni 2023, hata hivyo, kutokana na wajumbe wa jukwaa hilo kuwa na majukumu mengine ya kitaifa kikao hicho hakikuweza kufanyika na kiliahirishwa mpaka kitakapopangwa tena na kinategemea kufanyika mwezi August 2023. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kipindi hiki ilifanikiwa kufanya vikao vya Jukwaa la Haki Jinai ngazi ya Wilaya na Mikoa yote nchini ambapo wajumbe wa majukwaa hayo walijadili changamoto mbalimbali za haki jinai zilizopo katika maeneo yao na jinsi ya kuzitatua na kisha kuwasilisha taarifa za vikao hivyo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Haki Jinai Taifa.

Pia katika kipindi husika OTM ilifanikiwa kufanya uhamishaji wa majukwaa ya haki jinai na kutoa elimu juu ya umuhimu wa ufanyikaji wa vikao vya Jukwaa la Haki Jinai Wilaya katika Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa. Aidha, katika kuhakikisha kuwa vikao hivyo vinafanyika kwa ufanisi Mkurugenzi wa Mashtaka ametoa Waraka Na. 2 wa Mwaka 2023 kuhusu Uendeshaji wa Vikao vya Jukwaa la Haki Jinai ikiwa ni pamoja na usimamizi wa vikao vya majukwaa hayo, kalenda za vikao, taratibu za uendeshaji na wajibu wa vikao husika katika kila ngazi.

#### 4.7.4. Vikao Kazi kati ya Menejimenti na Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa

Katika kipindi cha Januari, 2023 – Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imefanikiwa kufanya vikao viwili (2) vya Menejimenti na Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa, Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi kati ya Aprili, 2023 na Juni, 2023. Kikao kimoja kilifanyika mkoa wa Morogoro na kikao kingine kilifanyika Dodoma. Vikao hivyo vilihusisha wajumbe 26 wa Menejimenti pamoja na Wakuu wa Mashtaka kutoka katika Mikoa 30 ya Kimashtaka na Wakuu wa Mashtaka wa Wilaya 62 pamoja na Waendesha Mashtaka Viongozi (PAI) 31.

Lengo Kuu la vikao kazi hivyo ilikuwa ni kufanya tathmini ya ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi na kutafuta suluhu za changamoto zilizopo katika utendaji kazi wa kila siku. Taarifa taarifa kuhusiana na muda wa upelelezi ambao ulikubaliwa usizidi siku 90, hali ya magereza na kuangalia kwa kiwango gani tumeweza kupunguza mlundikano wa mahabusu magerezani zilipokelewa na kujadiliwa. Pamoja na mambo mengine malengo mengine yalikuwa ni kupata taarifa ya namna ya uendeshaji wa kesi za madawa ya kulevya, na namna bora ya kuendesha kesi hizo kwa weledi na kupata mafanikio.

Katika kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, maazimio mbalimbali yalipitishwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mashauri yaliyopo Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi yanamalizika ndani ya kipindi cha miezi sita tangu kusajiliwa mahakamani. Pia, kufanya ukaguzi wa Vituo vya Polisi na Magereza na kufanya mapitio ya majalada ili kuhakikisha upelelezi wa mashauri unakamilika na maamuzi yanatolewa kwa wakati. Vilevile, Wakuu wa Mashtaka ngazi ya Mkoa na Wilaya walielekezwa kuongeza nguvu katika uratibu wa upelelezi na kuzingatia Muongozo Na.1 wa Mwaka 2023 wa Mkurugenzi wa Mashtaka wa utoaji taarifa na mrejesho wa kesi zilizoisha mahakamani na kuhakikisha majalada ambayo upelelezi wake umezidi siku tisini (90) yanakamilika kwa wakati.

### 4.7.5. Ukaguzi wa Shughuli za Mashtaka

#### 4.7.5.1. Ukaguzi wa Ofisi za Mikoa

Katika kipindi husika, Ofisi ilifanya ukaguzi wa Ofisi za Mikoa ambapo lengo la ukaguzi huo pamoja na mambo mengine ilikuwa ni kukagua na kufanya tathmini ya utekelezwaji wa shughuli za kimashtaka katika ngazi za mikoa na wilaya nchini. Kupitia ukaguzi huo, Ofisi imeweza kubaini kiwango cha utekelezaji wa miongozo ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa ni kizuri.

Aidha, ukaguzi ulibaini baadhi ya changamoto zinazokabili utekelezaji wa majukumu katika ngazi ya mikoa. Vilevile, Ofisi imepata maoni ya namna bora ya kutatua changamoto zilizobainika kwa lengo la kuboresha utendaji kazi kwa maslahi mapana ya Taifa. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja

na ufinyu wa vitendea kazi, ukosefu wa miundombinu ya majengo ya ofisi na nyumba kwa watumishi na uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala mazima ya Haki Jinai nchini.

## 4.8. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

### 4.8.1. Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Mikoa Kumi (10)

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2023 hadi Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imeendelea na utekelezaji wa ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Makao Makuu na Ujenzi wa Majengo Kumi ya Kimashtaka na ipo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo;

i. Jengo la Makao Makuu – Njedengwa: Kiwanja Na. **103**, Kitalu BA; eneo la Njedengwa ambapo utagharimu Shilingi **18,771,230,478.22.** Utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 45.15** kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 6,481,204,530.83.**

ii. Jengo la Mkoa wa Morogoro – Kiwanja Na. **51**, Kitalu X; Manispaa ya Mororgoro ambapo utagharimu Shilingi **1,489,443,717.12.** Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 74 kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 790,265,891.07**. Kazi ya ujenzi imaendelea.

iii. Jengo la Mkoa wa Ilala (Kinyerezi) – Kiwanja Na. 219, Kitalu B; Eneo la Kinyerezi- Dar es Salaam ambapo utagharimu **Shilingi 1,500,000,000.** Utekelezaji wa mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na Ofisi zimeanza kutumika.

iv. Jengo la mkoa wa Pwani – Kiwanja na. 221, Kitalu B; Eneo la Kibaha ambao utagharim **Shilingi 1,553,911,148.** Utekelezaji wa mradi huo umekamilika kwa asilimia 100. Jengo husika limeanza kutumika.

v. Jengo la mkoa wa Mbeya – Kiwanja Na. **2656**, Kitalu “M”, Eneo la Jiji la Mbeya ambao utagharim **Shilingi 1,594,535,431.** Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 74** kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 867,784,734.96**. kazi ya ujenzi inaendelea.

vi. Jengo la Mkoa wa Shinyanga – Kiwanja Na.150, Kitalu ‘S’ Eneo la Uzunguni-Shinyanga ambao utagharim **Shilingi 2,153,851,067.** Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 68 kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 907,857,875.17.** Kazi ya ujenzi inaendelea**.**

vii. Jengo la Mkoa wa Manyara – Kiwanja Na. 24, Kitalu ‘V’ Eneo la Negamsi-Manyara ambao utagharim **Shilingi 2,125,977,109.** Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 70 kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 1,004,537,843.29.** Kazi ya ujenzi inaendelea**.**

viii. Jengo la Mkoa wa Njombe – Kiwanja Na. 4, Kitalu ‘D’ Eneo la Lunyanyu - Njombe ambao utagharim **Shilingi 2,230,000,000.** Utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 30** kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 631,664,433.46.** Kazi ya ujenzi inaendelea**.**

ix. Jengo la Mkoa wa Rukwa – Kiwanja Na. 68, Kitalu ‘P’ Eneo la Sumbawanga - Rukwa ambao utagharim **Shilingi 2,246,327,795.** Utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 30** kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 619,405,938.24.** Kazi ya ujenzi inaendelea**.**

x. Jengo la Mkoa wa Katavi – Kiwanja Na.253, Kitalu ‘FF’ Eneo la Ilembo-Katavi ambao utagharim **Shilingi 2,337,053,227.** Utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 30** kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 634,305,045.85.** Kazi ya ujenzi inaendelea**.**

xi. Jengo la Mkoa wa Geitai – Kiwanja Na. 196, Kitalu ‘A’ Eneo la Magogo - Geita ambao utagharim **Shilingi 2,340,000,000**. Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 30 kukamilika na gharama zilizotumika mpaka sasa ni **Shilingi 606,113,725.81**. Kazi ya ujenzi inaendelea.

#### 4.8.2. Utekelezaji wa Programu ya Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania

Katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imetekeleza Programu ya Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania - BSAAT).

i. Machi, 2023 Ofisi ilifanyika mafunzo elekezi kwa Waendesha Mashtaka na Wapelelezi mkoani Morogoro juu ya ushughulikiaji wa makosa makubwa ya uhalifu wa kupangwa (Organised Crime Groups). Mafunzo haya yamewawezesha Waendesha Mashtaka na Wapelelezi kutoka mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam kupata uelewa wa kutosha wa namna ya kuainisha makundi ya uhalifu na kushughulikia makosa makubwa ya uhalifu wa kupangwa;

ii. Machi, 2023 Ofisi ilifanya ukaguzi katika mikoa Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam ambayo Mpango wa BSAAT unatekelezwa ili kupima utekelezaji na uzigatiwaji wa Mwongozo wa Uchunguzi na Uendeshaji wa Mashtaka ya Kesi Kubwa za Rushwa na Kesi Nyingine. Ukaguzi ulifanyika katika Ofisi za Taifa za Mashtaka (OTM) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika Mikoa ambayo ipo ndani ya Program ya BSAAT (Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam). Lengo la kufanya ukaguzi lilikuwa ni kufanya tathmini ya uzingatiwaji na utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa kwenye mwongozo katika hatua ya uchunguzi, kupitia majalada kwa ajili ya kufanya maamuzi, ufunguaji na uendeshaji wa mashtaka;

iii. Mwezi Februari na April, 2023 Ofisi iliandaa vikao kazi viwili (2) kwa lengo la kuwakutanisha wataalam kwa ajili ya kujadili na kuthibitisha Rasimu za Mwongozo wa Kitendaji wa Utaifishaji na Urejeshaji Mali Zilipopatikana katika Uhalifu (Asset Forfeiture and Recovery Guideline), Mwongozo wa Kuwajali na Kuwalinda Mashahidi (Witness Care and Protection Guidelines) pamoja na Usaidizi wa Kisheria wa Pande zote katika Masuala ya Jinai (Mutual Legal Assistance in

Criminal Matters) kwa Waendesha Mashtaka na Wapelelezi. Lengo la Miongozo hii ni kuwawezesha Waendesha Mashtaka na Wapelelezi kuwa na uelewa wa kutosha wa sheria ya ulinzi wa mashahidi, urejeshaji na utaifishaji mali pamoja na ushughulikiaji wa maombi ya usaidizi wa kisheria wa pande zote katika masuala ya jinai; na

iv. Mwezi Juni, 2023 Ofisi imefanya ukaguzi na mafunzo ya kuhusu matumizi ya Muongozo wa Uchunguzi na Uendeshaji wa Mashtaka ya Kesi Kubwa za Rushwa na Kesi Nyingine katika Mkoa wa Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam ambayo Mpango wa BSAAT unatekelezwa. Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uwezo Waendesha Mashtaka na Wapelelezi katika kutekeleza majukumu ya kiutendaji katika upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kama yalivyoainishwa kwenye Muongozo tajwa.

#### 4.8.3. Utekelezaji wa Mradi wa Haki Mtoto

Mwezi Disemba hadi Januari, 2022 Ofisi kwa kushirikiana na Mradi wa Haki Mtoto unaofadhiliwa na Shirika la UNICEF imefanya ukaguzi wa magereza 21 katika Mikoa 20 ya Kimashtaka ambapo watuhumiwa wa kesi wanazuiliwa. Lengo la ukaguzi huo pamoja na mambo mengine ni kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa ya ukaguzi wa watoto waliopo katika vizuizi uliofanyika mwezi November, 2021.

Aidha, Aprili, 2023 Ofisi kwa kushirikiana na UNICEF iliandaa Mwongozo wa Uendeshaji wenye Viwango (SOPs) katika mashauri ya watoto wanaokinzana na sheria na kutoa mafunzo elekezi kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka. Jumla ya Waendesha Mashtaka na Wpelelezi wapato 166 walishiriki katika mafunzo juu ya Mwongozo wa Uendeshaji wenye Viwango (SOPs). Lengo la muongozo na mafunzo hayo ilikuwa ni kuboresha ushughulikiaji wa makosa ya kubaka na mengine yenye asili ya kujamiiana ili kupunguza makosa hayo katika jamii.

## 5. MAFANIKIO

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023 kwa Ofisi ya Taifa ya Mashataka (OTM) ni kama ifuatavyo: -

i. Kuokolewa kwa fedha taslimu **Shilingi 1,455,698,000** na Dola za Kimarekani 2,064 na baadhi ya mali kama vile magari 11, pikipiki 64 na viwanja saba (7). Mali hizi zinazohusiana na uhalifu ambazo zimetaifishwa na kurejeshwa Serikalini kufuatia mashauri ya jinai yaliyomalizika katika mahakamani mbalimbali nchini;

ii. Kupunguza mlundikano wa mahabusi kwa kuwaachia huru mahabusi 1,603 waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka ya jinai, kupitia kaguzi za magereza, na Vituo vya Polisi pamoja na mapitio ya majalada na kaguzi za utendaji kazi katika Ofisi za Mashtaka Mikoa na Wilaya;

iii. Kusogeza huduma kwa wananchi kupitia kuongeza Ofisi katika Wilaya za Mashtaka 50 na kufanya Ofisi za Wilaya za Kimashtaka kufikia 94 nchini;

iv. Kupungua kwa malalamiko dhidi ya Serikali kutoka kwa watuhumiwa na wananchi kufuatia ziara na kaguzi zinazofanywa na OTM katika maeneo ambapo mahabusi wanahifadhiwa na kutatua changamoto zinazowakabili kwa mujibu wa Sheria; na

v. Kuendelea kuimarika kwa mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa katika mapambano dhidi ya uhalifu ikiwemo kuzuia wahalifu kunufaika na uhalifu, kubadilishana nyaraka za ushahidi na kushiriki katika mikutano nje ya nchi iliyoandaliwa na jumuiya za kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya haki jinai.

## 6. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Januari, 2023 hadi Juni, 2023, bado zipo changamoto zinazoathiri utekelezaji wa Malengo ya Kimkakati yaliyopangwa na kupunguza tija. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

i. **Ufinyu wa Bajeti**

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliomba kutengewa kiasi cha **Shilingi 99,506,862,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, Ofisi ilitengewa kiasi cha **Shilingi 45,262,695,000** ambacho ni sawa na asilimia **45.5** ya mahitaji halisi yaliyopendekezwa. Wakati kwa mwaka wa fedha 2023/24 kiasi kilichoombwa kilikuwa ni **Shilingi 163,074,874,560** na kiasi kilichoidhinishwa ni **Shilingi 68,858,929,000** pungufu kwa **asilimia 42.2** ya mahitaji halisi. Upungufu huu, utasababisha changamoto katika utekelezaji wa majukumu na kutofikia kwa malengo ya kimkakati yanayotarajiwa.

ii. **Usalama kwa Watumishi**

Watumishi hususan Mawakili wa Serikali na Makatibu Sheria wamekuwa wakishughulikia kesi mbalimbali zenye masilahi mapana ya Umma/jamii kama vile kesi za uhalifu wa kimtandao, uhujumu uchumi, dawa za kulevya na ugaidi. Katika kushughulikia kesi hizo wamekuwa wakikumbana na mazingira yanayohatarisha maisha kutokana na kuishi maeneo yasiyosalama, kutokuwa na uhakika wa vyombo vya usafiri pamoja na kutokuwepo kwa fedha za kulipa posho maalum ya kujikimu kwa Mawakili wa Serikali wanaoendesha kesi zenye mazingira ya kipekee na hatarishi.

iii. **Upungufu wa Rasilimali Watu**

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kuweza kutekeleza muundo na majukumu yake ipasavyo, ilipaswa kuwa na **watumishi 5,725** ifikapo mwaka wa fedha 2021/2022. Hata hivyo, hadi sasa OTM ina jumla ya **watumishi 915** na kuwa na upungufu wa **watumishi 4,810.**

iv. **Maslahi Duni kwa Watumishi**

Watumishi wanakabiliwa na maslahi duni hali inayosababisha kushuka kwa morali ya kufanya kazi na hivyo baadhi yao kuamua kuacha kazi na wengine kuomba kuhamia Taasisi nyingine za Umma zenye maslahi bora zaidi.

v. **Upungufu wa Vitendea Kazi na Majengo**

Ili kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inapaswa kuwa na majengo ya **Ofisi 169** katika mikoa na wilaya zote ambayo

Ofisi inafanya kazi. Kwa sasa Ofisi ina **Majengo Manne (4)** tu katika **Mkoa wa Iringa, Ilala, Pwani** na **Wilaya ya Serengeti**. Hivyo, Ofisi ina upungufu wa jumla ya **majengo 164** ikiwemo jengo la Makao Makuu, **Ofisi za Mikoa 28** na **Wilaya 136**. Vilevile, Ofisi ina upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, samani za ofisi, vitabu vya sheria, kompyuta na mashine za kutoa nakala katika ngazi ya Makao Makuu, Mikoa na Wilaya.

**vi. Kuongezeka kwa aina Mpya ya Uhalifu na Matukio Yanayohatarisha Usalama wa Wananchi**

Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yamesababisha kuibuka kwa aina mpya za uhalifu unaotumia teknolojia hizo. Mbali ya makosa mapya kama ugaidi na utakatishaji fedha. Aidha, wahalifu wameweza kubuni mbinu mpya za kutenda makosa ya asili kama vile wizi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na makosa ya kughushi kwa kutumia teknolojia.

**vii. Ulinzi kwa Watoa Taarifa na Mashahidi**

Kwa sasa hakuna skimu na programu ya kuwalinda watoa taarifa na mashahidi katika mfumo mzima wa Haki Jinai. Hali hii imesababisha watoa taarifa na mashahidi kutokutoa ushirikiano kwa vyombo vya haki jinai kwa kuhofia usalama wao.

## 7. MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

Katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa Sehemu ya Sita hapo juu, mambo yafuatayo yanafanyika: -

i. Kuendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuongezewa ukomo wa bajeti ili kuendana na mahitaji halisi ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi kama yalivyoainishwa kwenye muundo;

ii. Kuendela kuomba vibali vya ajira kwa wakati ili kukabiliana na upungufu wa watumishi;

iii. Kuendela kujenga hoja kwa Serikali ili kuboresha maslahi na mazingira ya kazi ya watumishi ili kuwajengea morali na kuwawezesha kuishi maeneo yenye usalama zaidi;

iv. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi wa Ofisi za Mashtaka za Mikoa, Wilaya na Nyumba za Watumishi;

v. Kuwepo na Programu Maalumu ya Mafunzo kwa Watumishi wa OTM ili kukabiliana na aina mpya za uhalifu;

vi. Kuwekwa kwa utaratibu wa ulinzi kwa watoa taarifa na mashahidi katika mfumo mzima wa Haki Jinai;

vii. Kuanzisha Kituo cha Umahili kwa ajili ya Waendesha Mashtaka ili kuboresha utendaji kazi; na


viii. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Mashtaka.

## 8. HITIMISHO

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni mdau muhimu katika usimamizi wa haki jinai nchini. Kwa kuzingatia umuhimu wa Utawala Bora na Utawala wa Sheria katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa na amani na usalama, ni vyema Serikali ikaendelea kuimarisha Ofisi hii ili kutimiza Dira na matarajio ya Taifa. Dira ya OTM ni ***'Haki, Amani na Usalama kwa Maendeleo ya Taifa'.*** Ni matumaini yetu kuwa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali itaendelea kuimarishwa zaidi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi na hivyo kuwahudumia wananchi kikamilifu. Ofisi itaendelea kudumisha Dhima yake kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi ili kuifikia Dira yetu.

## Kiambatisho Na. 1: Muundo uliopitishwa wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

*(Umepitishwa na Rais tarehe 07 Julai, 2018)*



**Kiambatisho Na. 2: Taarifa ya Magereza na Vituo vya Polisi Vilivyotembelewa Julai, 2022 hadi Disemba, 2022**

| Na. | Mkoa | Magereza Yaliyotembelewa | Vituo vya Polisi Viliyotembelewa | Idadi ya Mahabusi Walioachiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 1 | 3 | 8 |
| 2 | Dar es Salaam | 4 | 0 | 67 |
| 3 | Ilala | 1 | 9 | 17 |
| 4 | Kinondoni | 1 | 12 | 7 |
| 5 | Temeke | 4 | 3 | 127 |
| 6 | Dodoma | 6 | 3 | 50 |
| 7 | Geita | 2 | 15 | 27 |
| 8 | Iringa | 2 | 5 | 3 |
| 9 | Kagera | 5 | 7 | 7 |
| 10 | Katavi | 1 | 2 | 5 |
| 11 | Kigoma | 3 | 8 | 470 |
| 12 | Kilimanjaro | 3 | 3 | 0 |
| 13 | Lindi | 5 | 5 | 248 |
| 14 | Manyara | 3 | 1 | 34 |
| 15 | Mara | 3 | 4 | 33 |
| 16 | Mbeya | 11 | 8 | 0 |
| 17 | Morogoro | 3 | 10 | 2 |
| 18 | Mtwara | 1 | 4 | 6 |
| 19 | Mwanza | 4 | 14 | 11 |
| 20 | Njombe | 3 | 3 | 44 |
| 21 | Pwani | 10 | 9 | 235 |
| 22 | Rukwa | 3 | 3 | 63 |
| 23 | Ruvuma | 1 | 4 | 0 |
| 24 | Shinyanga | 2 | 10 | 11 |
| 25 | Simiyu | 5 | 2 | 69 |
| 26 | Singida | 1 | 2 | 14 |
| 27 | Songwe | 1 | 3 | 3 |
| 28 | Tabora | 5 | 8 | 13 |
| 29 | Tanga | 8 | 3 | 27 |
| 30 | Tarime | 1 | 5 | 2 |
| **Jumla** | | **103** | **168** | **1,603** |